

KRISTO ALIYETAMBULISHWA

KATIKA NYAKATI ZOTE



Asante, ndugu. Mwaweza kuketi. Hakika ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu usiku huu, kuwa hapa Louisville, Mississippi. Tumeutarajia wakati huu, kwa muda mrefu sana, nami nilifikiri ya kwamba ningeenda Louisville. Natokea tu upande wa pili wa mto kutoka Louisville, Kentucky, makazi ya uenyeji wangu. Inaonekana kama ni kuja nyumbani tena, kuwako huku Louisville.

Sasa, huko juu, baadhi yao huuita “Luavul,” “Louis-ville,” na “Lueyville.” Nami sijui unaitwaje hapa. Nafikiri sisi, njia bora kabisa, vile nilivyouita siku zote, ilikuwa ni Louis-ville. Inaonekana kana kwamba L-o-u-i-s- lingekuwa Louis-ville. Lakini, huko nyumbani ni “Luavul,” na “Lueyville,” na “Louis-ville,” kwa hiyo tunajichagulia tu, lile tunalotaka kutumia.

Jambo muhimu ni, kwamba, tumekusanyika pamoja katika Jina la Bwana Yesu. Tumekusanyika hapa si kwa kusudi lingine bali kumtumikia Yeye, na kwamba Jina Lake kuu lipate kuheshimiwa miongoni wetu, zaidi. Wakati tukiwa... Mkutano utakapokwisha, basi ingewezekana... Inawezekana, kama ambavyo ingaliwezekana sasa. Tunajua ya kwamba tunamheshimu kwa moyo wetu wote.

Na sasa nimekuja hapa kwa mwaliko wa wahudumu wa hili, eneo hili lote hapa, na mahali hapa. Nami nimekuja bila jambo la tofauti na lao; ni Injili ile ile tu. Ninaamini, Yesu alisema wakati mmoja, ya kwamba, “Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu aliyechukua ja—jarife na akaenda baharini. Na wakati alipolitupa, alivuta kila namna.” Sasa, hivyo ndivyo tunavyopata katika jarife la Injili.

Mtu anapotupa jarife baharini ama ziwani, ni vigumu kwake kujua atakachopata kutoka humo. Kwa sababu, angeweza kupata kamba. Na angeweza kupata samaki mla mizoga. Angeweza kupata buibui, nyoka, na—na chochote kile zaidi.

Lakini, ni kazi yetu kuvua kwa juya. Si kazi yetu kuhukumu. Nami ninakuja kuchukua jarife langu, ambalo Bwana amenipa, na kuliunganisha na majarife ya watu hawa, kusudi, sisi, majarife mawili yatafika mbali kidogo kuliko jarife moja litakapofikia. Kwa hiyo, nimeunganisha jarife langu na ninyi ndugu hapa. Ninyi watu wote hapa, ambao ni washirika wa makanisa ya hapa, nimeunganisha jarife langu nanyi, tupate kuyatupa baharini hapa, na tuyavute na tuone kama Bwana ana wengine—wengine hapa chini ambao bado hawajashikwa.

Na Injili kuu ya Bwana wetu Yesu Kristo itambulishwe vizuri sana miongoni mwetu, katika siku hizi zingine tano usiku hapa, tupate kuona hao wote ambao hawajashikwa, katika wakati huu, wapate kushikwa katika ja—jarife la Injili, kwa matumizi ya Bwana.

Sasa, sisi, hili haliwezi kufanywa peke yake, peke yake. Halina budi kufanywa kwa ushirikiano na maombi, na sisi sote pamoja, kuungana pamoja na kuiweka mioyo yetu pamoja, na kuomba.

Na sasa tumefurahia uamsho wa karibu miaka kumi na mitano, ambao kulingana na historia ni mrefu kuliko uamsho wowote ulivyopata kudumu, ni juavyo mimi. Kwa kawaida, uamsho hudumu kwa muda wa kama miaka mitatu hivi, ndipo unatawanyika. Lakini nikiamini ya kwamba huu ni mmoja wa miamsho mikuu sana ya mwisho ambayo ulimwengu utapokea, na umekuja katika wakati wa mwisho, wakati wa Laodikia, mwishoni mwa kipindi cha wakati wa Kipentekoste. Nami ninaamini kanisa sasa linaingia katika uvuguvugu wake, kama Biblia ilivyobashiri. Nasi tunaona kushikwa tu kwa ile sehemu ya mwisho, tunapoonamambo yakitendeka kama vile yamekuwa yakitendeka ulimwenguni, katika siku chache zilizopita.

Kwa mfano, lile tetemeko kuu la Alaska. Hapajakuwapo na tetemeko kama hilo, ulimwenguni kote. Mliona? Lilitokea katika Ijumaa Kuu. Mwajua, mara ya mwisho ulimwengu ulipotikiswa ilikuwa ni katika Ijumaa Kuu, pia, wakati Bwana wetu alipokufa, na liliutikisa ulimwengu mzima. Na kumbukeni, huenda ikawa ni ishara ya Yeye kurudi. Yeye alisema, ya kwamba, “Kutakuwako na matetemeko ya nchi mahalihali.” Leo hii tumepata lingine huko California, nayo yanatokea tu kila mahali, matetemeko mepesi. Tunaona, hata jengo la Makao makuu limetoka mahali pake, na kurudi nyuma. Na—na hapa chini katika Baton Rouge, Louisiana, kuna bwawa la kuogelea kule, liliyarusha maji nje, moja kwa moja kutoka Alaska. Huko Switzerland, Sweden, na kote kule, nyumba zilitikiswa na kadhalika, kote ulimwenguni.

Ninaamini hilo linajaribu kuyafungua macho yetu, kuona saa tunayoishi. Niko hapa katika hofu ya Kiungu, ya kwamba, huenda ikawa kumekaribia sana kuliko tunavyowazia, kule kuonekana Kwake.

Na ndugu na dada, hata kwa vijana, hebu na tuweke uaminifu wote tunaoweza. Huenda huu ukawa ndio uamsho wa mwisho tutakaowahi kuhudhuria, na huenda tusiumalizie huu, mpaka kufikia Kuja Kwake. Ninamtazamia Yeye leo. Kama hakuja hapa leo, nitakuwa nikimtazamia kesho, kama nikiwepo hapa. Na nimekuwa nikimtazamia sasa, tangu niliposikia kuhusu kurudi Kwake, na hiyo imekuwa ni miaka thelathini na mitatu iliyopita wakati nilipompa moyo wangu. Nimekuwa

nyuma ya mimbara, miaka thelathini na mitatu, nikijaribu na kuutangaza utajiri usiopimika wa utukufu Wake. Nami ninatumaini ya kwamba Mungu atajitambulisha sana miongoni mwetu, hata kila asiyeamini ataokoka, na wagonjwa wote wataponywa, na watakatifu wa Bwana, watoto Wake waaminio, watainuliwa juu katika—katika Roho.

Uamsho haumaanishi kuwapata washiriki wapya. Ni kuwaamsha wale tulio nao tayari. Unaona? Ni kuamsha.

Nilisimama, wakati fulani uliopita, na kuangalia mawimbi kwenye Ziwa Michigan, nikiona, nilipokuwa nimesimama pale, baada ya uamsho mkuu huko Chicago. Niliona ma—mawimbi, jinsi yalivyokuwa yakiingia, katika wimbi kubwa tu, yakiingia tu kasi na kutoka. Nikawaza, unajua, inanikumbusha juu ya ule wimbo, “Mafuriko ya furaha nafsini mwangu, kama mawimbi makubwa ya bahari yakifingirika.” Na mawimbi hayo huanzia mahali fulani, huko kwenye hilo ziwa ama baharini. Nayo yanapokuja, yanaongeza nguvu mwendo, wakati wote. Ndipo, hatimaye, yanapiga ufuko; yanatoka tu, yapate kurudi tena.

Na hivyo ndivyo mawimbi ya utukufu wa Mungu yanavyofanya. Yanaingia, kama tu—kama tu wimbi refu, linafingirika na kufingirika, nyuma kwa nyuma, na nyuma na mbele, mawimbi ya furaha ya Mungu yanavingirika kupitia nafsini mwetu.

Nashangaa, “Hiyo ilikuwa na faida gani? Kuna manufaa gani ya kutibuatibua maji juu chini?” Maumbile yana njia za kujishughulikia.

Ni kama tu watu, sasa, wakati mnapokuwa kanisani mwenu na wachungaji wenu, mnapokuwa na somo la shule ya Jumapili ama—ama kitu fulani kanisani mwenu. Labda hakuna msisimko unaoendelea, ama—ama kitu chochote kisicho cha kawaida. Lakini, bado, kuna Mungu moyoni mwako kadiri kulivyo wakati mnarukaruka juu chini ama kupaza sauti.

Niliwaza, “Kwa nini wanafanya hivyo?” Sababu iyo hiyo Mungu aliyo nayo, uamsho, ndiyo sababu iyo hiyo Yeye huweka uamsho baharini, huweka uamsho ziwani. Na maji, kutibuka kuumuka kwenda juu na kurudi chini, yanaondoa takataka zote kutoka kwenye maji, yanazitupa ufukoni. Nami nafikiri hilo ni jambo zuri, ya kwamba tuna miamsho, na kwa namna fulani tunatupilia mbali ushirikina wote kutoka kwetu, na u—u—ulimwengu wote kuutoa nje, kuutibua utoke, na kuutupilia nje ufukoni, kusudi maji yasiwe na vitu kama hivyo.

Sasa, usiku wa leo, kwa namna fulani ni ninii... Mara yangu ya kwanza niliyopata kuwa hapa, na hata hivyo sijisikii mimi ni mgeni miongoni mwenu. Si—si mgeni. Mimi ni ndugu yenu. Na mimi—na mimi, hakika, upya wa kufahamiana tu sisi kwa sisi... Labda, baadhi yenu, ninajua sijapata kuwaona. Labda hamjapata kuniona. Na daima kuna ile hisi ndogo ngumu

ambayo mtu unaninii tu...Ni vigumu. Nasi tunaninii tu... Mambo yako hivyo tu, sasa, kila mahali. Ninafanya, ninaanza safari yangu ya nane ya kuuzunguka ulimwengu. Nami ni—ni—ninapata jambo hilo, kila mahali, haidhuru uko wapi.

Lakini unapowapata Wakristo, mahali Roho Mtakatifu alipo, haidhuru ni taifa gani, ni umbali gani huko msituni, ama popote pale, wao wanafanya jambo lile lile mnalofanya mnapompokea Roho Mtakatifu. Wanafanya jambo lile lile kabisa. Wana uhuru ule ule walio nao. Wanaamini vile vile na wanafanya vile vile Mkristo ye yote anavyofanya anapompokea Kristo.

Lakini, hapo ndani, unapata ugumu huo. Na, nafikiri, usiku wa kwanza ni wakati mzuri wa kufahamiana kwa namna fulani. Halafu, sasa, basi, wakati mkutano ukiendelea na kufanikiwa, basi tutafahamiana zaidi sisi kwa sisi kuliko vile tulivyo sasa. Lakini, kadiri tutakavyotoka upesi kwenye hilo, mbona, ndivyo tutakavyokuwa na heri zaidi.

Roho Mtakatifu ni mwepesi kujitenga, ni mwepesi sana kughairi, sana. Na—na mnapokuwa na asiyeamini mmoja tu ama mwenye kushuku ameketi mahali hapo, Roho Mtakatifu kamwe hatafanya kazi, ni vigumu. Kumbukeni, Yesu alimwongoza mtu mmoja moja kwa moja akamtoa nje ya mji, apate kumponya, wakati mmoja, kumwondoa kutoka kwenye kutokuamini. Aliingia katika mji Wake Mwenyewe, na Biblia ilisema, “Wala asingeweza kufanya miujiza mingi mikubwa.” Hatutaki kuliwazia jambo hilo hivyo, bali Biblia ilisema hakuweza kuifanya. Unaona? Yeye hawezi kufanya jambo lolote kinyume na imani yako. Ni lazima uamini.

Mtu fulani ameniambia, mara nyingi, akisema, “Ndugu Branham, sijali kile kingetukia; Siamini jambo hilo.” Vema, halikuwa ni kwa ajili ya mtu huyo.

Hilo si kwa wasioamini. Ni kwa waaminio tu, hao waaminio. “Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.” Wasioamini hawapati kitu chochote. Na kwa hiyo ha—hawaamini chochote, kwa hiyo hawapati kitu. Kama wana theolojia baridi tu, hilo ndilo wanalopata. Bali wale wanaomwamini Mungu, na wanaamini ya kwamba Yesu Kristo ni halisi tu leo kama alivyowahi kuwa, hicho ndicho wanachopokea. “Kulingana tu na imani yako, na iwe kwako.”

Halafu humu ndani, niliwaza nitatoa, usiku wa leo, kile tunachojaribu kufanya.

Sasa, nakisia, kwa kuwa huu umedhaminiwa na Pentekoste, hivyo wengi humu ndani ni Wapentekoste. Na huko ndiko nilikotupa kura yangu, ingawa kamwe sikuwahi kujiunga na kanisa lolote la Kipentekoste, wala kanisa lolote. Sina dhehebu lolote, dhehebu fulani. Na, kwa kweli, siyathamini sana. Wanaweza kuwa na chochote watakacho. Lakini unachora

mstari, unaona, na Mungu—Mungu hapendi mipaka iwekwe katika Kanisa Lake.

Inanikumbusha juu ya jamaa mmoja, wakati mmoja, alikuwa na mabata, naye a—alikota mabawa yao kusudi wasiruke kutoka kwenye kizimba. Alikuwa amewaweka mabata upande mmoja, na mabata upande mwingine. Maji yakaanza kuingia. Muda si muda wajua, maji yaliendelea kupanda juu zaidi na zaidi, ndipo hao mabata wakawa pamoja basi. Unaona? Hivyo ndivyo tunavyohitaji kufanya. Hebu maji yaendeleo kupanda juu, na ndipo mabata watakusanyika pamoja, unaona, basi. Nasi sote tuko ndani ya maji yale yale. Kwa hiyo, vizuizi vya kimadhehebu vinaweza kuelea na kutolewa, kama tu tutaacha maji yapate kilindi cha kutosha.

Ni kama mtu aliyekuwa na shamba la mahindi. Jamaa fulani alishikilia kusema... Alikuwa na shamba moja, mimea inaelekea *huku*; na jingine mimea imeelekea *huku*. Na kwa hiyo jamaa aliyekuwa akiendesha ndege, kila asubuhi, angeangalia shamba hilo la mahindi. Akasema, “Lile si ni shamba zuri la mahindi *hapa*, na moja *pale*!” Baada ya hayo mahindi kuwa marefu kidogo zaidi, yakafikia kote kwenye ua, lilionekana kana kwamba ni shamba moja. Kwa hiyo ninatumaini itakuwa hivyo hapa, kwamba sisi ni shamba moja kubwa mno la mahindi, la moyo kwa moyo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

Sasa, kusudi letu.

Sasa, mara nyingi, watu husema, “Ndugu Branham, mponyaji wa Kiungu.” La. Hilo ni kosa. Kuna mponyaji mmoja tu; huyo ni Mungu. Hakuna dawa ambayo huponya, hakuna daktari ambaye ni mponyaji. Hakuna daktari mzuri anayedai kuwa ni mponyaji. Na kama akidai, basi yeye a—a—anakwambia jambo baya.

Nilihojiwa kwa Ndugu wa Mayo, nao wakasema, “Sisi hatudai kuponya wagonjwa, Bw. Branham. Tunadai tu kuyasaidia maumbile. Kuna mponyaji mmoja; huyo ni Mungu.” Na jinsi hilo lilivyo la busara!

Ungeweza kuuvunja mkono wako; daktari angeweza kuuweka vizuri. Bali asingeweza kuuponya, maana hana kitu cha kuponya. Ingeupasa kujenga tishu. Huenda daktari akang’oa jino ama akate kidole tumbo, bali ni nani atakayeponya? Unaona, Biblia haijakosea. Biblia ni sahihi katika kila Neno. “Mimi ni Bwana niyaponyaye magonjwa yenu yote.” Yote! Hakuna mwingine! Hakuna jambo muhimu. Bado hawajapata kitu ambacho kingeweza kujenga tishu. Wanapata dawa ambazo zingeweza kutia sumu virusi, mpaka—mpaka tishu zinashikana pamoja. Lakini, inahitaji Mungu, kuponya. Mungu ndiye mponyaji pekee aliyepo.

Kwa hiyo, Biblia ni kweli kikamilifu. Na hiyo ndiyo tunayosimama juu yake: Biblia. Haina budi kuwa ni BWANA

ASEMA HIVI. Sasa, tunaamini ya kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Neno Lake, kwa kuwa Yeye ni Mungu. Yeye hufanya lolote analotaka. Lakini, hata hivyo, ninapenda kuona chochote, wakati kinapopitia kwenye mstari wa fundisho, kinapotoka kwenye Biblia. Kwa sababu, ninaamini ya kwamba Biblia ni ufunuo kamili wa Yesu Kristo. Biblia ilisema hivyo ndivyo ilivyo. Ni Ufunuo wa Yesu Kristo. Wala hakuna kitu kinachopaswa kuongezwa Kwake, wala chochote kuondolewa Kwake. Kwa hiyo, ninapenda kudumu moja kwa moja na yale inayosema na yale inayoahidi. Kama Yeye angefanya tu yale aliyoahidi, hilo tu ndilo ninalojali kuona, haidhuru. Ndipo ninajua nitamwona.

Sasa, katika jambo hili hatujaribu kusema ya kwamba tunaweka umuhimu kwenye uponyaji wa Kiungu, kwa maana uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo. Wala usingeweza kuweka umuhimu katika jambo dogo. Lakini karibu asilimia themanini na sita, nafikiri ndivyo inavyokisiwa, ya huduma ya Yesu, ilikuwa ni kwenye Uponyaji wa Kiungu. Yeye. . .

Kama vile Dk. Bosworth alivyozea kusema, nanii wangu. . . Mmoja wa marafiki zangu ambaye ameenda Utukufuni hivi karibuni tu, miaka michache iliyopita, yapata. . . akiwa na umri wa karibu miaka themanini na minne. Yeye alisema, “Uponyaji wa Kiungu ni chambo kilichoko kwenye ndoana. Na kamwe mtu humwonyeshi samaki ndoana. Unamwonyesha chambo, kwa hiyo anameza chambo na kushikwa na ndoana.” Kwa hiyo, hivyo, hivyo ndivyo ilivyo. Tunataka kuwashika samaki kwa ajili ya utukufu wa Bwana; tuwashike watoke ulimwenguni, na kuwaingiza katika Ufalme wa Mungu.

Na kwa hiyo, uponyaji wa Kiungu, jambo muhimu ni uponyaji wa Kiungu wa nafsi. Mwili wa Kristo, unahitaji uponyaji kwa uzito zaidi ya kitu chochote nijuacho, ni Mwili wa Kristo. Umevunjwawunjwa sana na theolojia ya wanadamu na tofauti za madhehebu, mpaka umekuwa ni Mwili mgonjwa. Nami. . . Nami nawaambia, una—unahitaji uponyaji, uponyaji mkuu. Kwa hiyo na—natumaini ya kwamba Bwana atafanya jambo kuu kuhusu uponyaji wa sehemu ya Mwili Wake iliyo humu ndani.

Tunaamini ya kwamba kuna moja, Kanisa moja. Wala kamwe hatujiungi Nalo. Jumatatu ijayo, nitakuwa na umri wa miaka hamsini na mitano, wala familia ya Branham kamwe haikuniomba kujiunga na familia yao. Nilizaliwa Mbranham. Hivyo ndivyo—hivyo ndivyo nilivyo.

Sasa, hivyo ndivyo tulivyo Wakristo. Tumezaliwa Wakristo. Wala hamjiungi nao. Unazaliwa humo. Ndipo unachukua tabia ya Kristo.

Sasa, tunapata pia kwamba, katika jambo hili, watu wengi hapa Marekani, hasa, ambao wamefundishwa. Tuna mfumo,

ama, Bwa—Bwana aliliagiza, kwa hiyo ni zuri, juu ya kuweka mikono juu ya wagonjwa na kuwaombea. Hilo lilikuwa ndilo agizo la mwisho kwa kanisa. Hilo ni zuri sana. Na limetekelezwa, kote katika nyakati. Kila wakati uamsho ulipotokea katika wakati wowote, kulikuwa na uponyaji wa Kiungu ulioambatana nao, na miujiza ya Mungu.

Na sasa tunaona, katika wakati huu, na kujaribu kwangu, kile ninachojaribu kufanikisha, ni hiki. Kumekuwako na mengi sana katika siku hii ya mwisho, juu ya watu wanaohubiri uponyaji wa Kiungu, wameweka utukufu mwingi sana wa kibinafsi ndani yake, hata umetoa ladha mabaya mbele ya umma. Imekuwa ni, “Bwana abarikiwe! Ndugu *nanii* aliniwekea mikono, na, Bwana asifiwe, nikaponywa.” Sasa, laiti ningaliweza tu kuliacha hilo!

Kama mtu fulani angeweza kusema, “Bwana Yesu aliniponya,” jinsi hilo lingalikuwa ni bora zaidi, unaona. Kwa hiyo, kwa huduma ndogo ambayo Bwana amenipa, ni kujaribu kumleta Yeye mbele zenu, mpate kuweka mikono yenu juu Yake, Dhahihu yenu, na mponywe. Si sana sana kuweka mikono. Ambako, sisi hufanya, sisi sote. Tunaomba na kuweka mikono juu ya wagonjwa.

Hatuwaponyi watu. Wameponywa tayari. Kila mtu ameponywa tayari. Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa hebu tuone jinsi kusanyiko letu limekwisha fundishwa. Kuna theluthi mbili za hao wanaoamini hilo, hata hivyo. Sasa, hilo, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Kila sifa aliyoifia, pale Kalvari, ni yetu tangu wakati huo na kuendelea, kila kitu alichokifia. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Tuliponywa, wakati uliopita.

Kila mwenye dhambi ameokolewa. Tangu siku ambayo Yesu alikufa msalabani, Yeye alisamehe kila dhambi ya mwanadamu.

Sasa, Mungu ni *nanii* mkuu—*nanii* mkuu... kama Mwenye Uhai mkuu. “Hapo mwanzo Mungu...” Mnaona? Sisi... Yeye hata hakuwa ni Mungu, kwanza. *Mungu* ni “kitu cha kuabudiwa.” Naye aliitwa... Hapakuwapo na kitu, cha kumwabudu. Yeye alikuwa Elohimu aliyeishi peke yake, wala hakukuwako na kitu chochote cha kumwabudu. Wakati alipowaumba Malaika, ndipo kukawa na kitu cha kumwabudu.

Bali katika Mungu huyu aliye mkuu, Elohimu, kulikuwako na sifa. Kulikuwamo humo na sifa kuwa Mungu; sifa za kuwa Baba; sifa za kuwa Mwana; sifa za kuwa Mwokozi; sifa za kuwa mponyaji. Sifa hizi zote zilikuwa ndani ya Mungu. Na kama ulipata kuwa na Uzima wa Milele, ulikuwa katika sifa za Mungu, kwa kuwa una Uzima wa Milele. Yesu alikuja kama

Mkombozi. Na *kukomboa* maana yake ni “kurudisha kitu mahali kilipoanzia.” Kweli. Ulikuwa katika mawazo ya Mungu. Huenda ilimlazimu kuzalisha *hiki* na *kile*, na *humu* chini na *humu* chini.

Ni kama mtu anayetengeneza kengele kwa ajili ya kanisa; anaweka kiasi fulani cha shaba na kiasi fulani cha chuma, na kuipa tu sauti inayofaa. Mfyanzi anajua jinsi ya kuiweka ndani. Kama hajui, hapati mlio unaofaa.

Naye Mungu anajua mahali pako hasa, na kwamba wewe ni wa wakati gani. Na, kwa hiyo, kama una Uzima wa Milele; Neno *Milele* ni “kitu ambacho kamwe hakikuanza, wala kamwe hakiwezi kwisha.” Kwa hiyo, vyovyote ulivyokuwa, unaona, ulikuwa, daima ulikuwa hivyo. Ulikuwa sifa ya Mungu iki—ikidhihirishwa, Ne—Neno. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno.”

Na neno ni wazo lililodhihirishwa. Unaliwaza, ndipo unalinena. Kama vile ningesema, “Nuru.” Ilinibidi kuwazia “nuru” kabla sijasema “nuru.” “Maikrofoni,” inanibidi kusema . . . kuwazia “maikrofoni,” nipate kusema “maikrofoni.”

Nasi ni sifa za Mungu zilizodhihirishwa.

Nami ninaona, ninapata matabaka mawili ya watu hili linapoendelea. Moja la hayo ni la kimsingi, na hilo jingine ni Wapentekoste. Sasa, Wapentekoste wana kitu fulani, bali hawajui wao ni akina nani. Nao wa kimsingi wanajua kitu fulani, bali hawana kitu kuendana nacho. Kwa hiyo sasa, hapo, ni kama tu mtu aliye na pesa katika benki, wala hawezi kuandika hundi. Huyu mwingine anaweza kuandika hundi; ila hana pesa katika benki. Kama ungeweza kuweka kitu hicho pamoja, lingekuwa—lingekuwa ni jambo kuu.

Lakini, sasa, unapokabiliwa na jambo hili, jinsi tunavyojaribu kuendelea mkutano, ni juu yako wewe, wewe kama mtu binafsi, kwa ajili ya haja yako katika Kristo. Wokovu, uponyaji wa Kiungu, ama chochote unachohitaji, ni kuninii, kwa imani, kujua ya kwamba wewe upo katika Uwepo wa Kristo, na kwa imani unyoshe mkono na kulipata. Kwa kuwa, hivyo ndivyo utakavyowahi kulipata. Ni . . . Kwa imani tumeokolewa. Kwa imani tunaponywa. Unaona? Si kitu ambacho kitamlazimu Mungu kushuka na kukifanya tena; Yeye amekifanya tayari.

Kwa hiyo, unaona, jambo hilo lote ni—ni, Mungu akifanyika mwili. Huyu, kwenye Siku ile kuu itakayokuja, wakati Kristo atakapoketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi na kutawala katika ule Utawala wa Miaka Elfu, ni Mungu, katika mwili, hapa duniani.

Yeye sasa yuko ndani yako. Wewe ni sifa Zake. Kama una Uzima wa Milele, uzima wako ulikuwako daima. Nawe ulikuwa ni mawazo ya Mungu: rangi ya nywele, chochote ulicho, ulikuwa ni mawazo ya Mungu, na umefanyika tu mwili.

Na hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa wakati alipofanyika mwili katika Kristo; Mungu, akiwekwa wazi, akidhihirishwa katika mwili, katika Kristo. Alifanyika mwili; Mungu ambaye tungeweza kumgusa. Timotheo wa Kwanza 3:16, “Bila shaka siri ya utauwa ni kuu: kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili.” Unaona? Unaona? Ilikuwa ni Mungu akidhihirishwa, akijifanya tayari.

Sasa, tupo hapa, katika umbo hili, tungali ni negetivu. Ni kama kupiga picha ya kitu fulani, na kuipiga. Mungu anasema, “Atakuwa na nywele nyeusi, macho ya bluu, na kadhalika. Atakuwa *hivi, vile*, ama *vinginenvyo*.” Picha inapigwa, umri wa kama miaka ishirini, ishirini na miwili.

Ndipo mauti yanaingia, unaanza kufa. Haidhuru unakula kiasi gani, jinsi unavyorudisha chakula vizuri mwilini mwako, kufanya seli za damu, unakufa. Wala hakuna mwanasayansi ulimwenguni anayeweza kuelezea jambo hilo.

Ulimwaga maji kutoka kwenye jagi, ukayatia katika bilauri, inajaa nusu; halafu unaendelea kuyamwaga, yanapungua. Vipi kuhusu jambo hilo?

Chakula unachokula hufanya seli za damu. Seli za damu huujenga mwili wako. Kila unapokula, unayafanya upya maisha yako. Ulipokuwa na umri wa mwaka mmoja, na kuendelea, ukaendelea mpaka ukafikia yapata miaka ishirini na miwili. Na ndipo basi, sasa, unakula chakula kile kile. Ninakula chakula kile kile nilichokula kwenye umri wa miaka kumi na sita. Kwenye umri wa miaka kumi na sita, kila ninapokula, kinajenga misuli na inakuwa mikubwa na yenye nguvu. Nikakomaa kabisa. Ndipo nikiisha kukomaa kabisa, ninakula chakula kile kile, hata kizuri zaidi, na kingi zaidi, nami ninaendelea kuzeeka na kudhoofika zaidi, wakati wote. Lakini kila wakati ninayafanya upya maisha yangu, basi isingenibidi kufa. Unaona?

Lakini Mungu amefanya miadi, na mwanadamu hana budi kufa na kuikabili Hukumu. Nanyi mtatimiza miadi hiyo, enyi marafiki. Kumbukeni hilo tu. Na wakati tukiwa hapa, usiku wa leo, tunataka kuyakumbuka mambo hayo, ya kwamba hatuna budi kutimiza miadi hiyo. Huenda kukawa na mingi mtakayosimama na kukwepa, lakini hilo ni moja tulilo na hakika nalo, kila mmoja, kutimiza. Na sasa, katika jambo hilo, ni miadi ambayo Mungu amefanya na mwanadamu. Mwili huu hauna budi, kwa maana ungali ni negetivu. Unapasiwa mauti.

Kwa hiyo, Yeye anapata Roho wa Milele, sifa Zake zikionyesha katika mwili huo, basi, kama picha yoyote katika hali yake ya negetivu, inayoingia kwenye chumba cha kusafishia picha. Hapo inasafishwa. Inatokea ikiwa picha kamilifu. Nasi tunaingia kwenye chumba cha kusafishia, bali kutoka baada ya negetivu kuwa picha kamilifu, katika mfano wa Kristo.

Tunaingia kwenye kaburi lenye giza, katika chumba chenye giza cha kusafishia. Inahitaji mauti kuisafisha.

Kama vile tu inavyochukua mauti, kwa nafsi yako, kuisafisha picha ya sura ya Kristo, uhai wa Kristo ndani yako. Inakupasa kutupilia yako nje, ili kwamba Kristo aweze kuingia ndani. Inakubidi kufa kwa nafsi yako.

Ndivyo na mwili wako wa kawaida unavyokufa, upate kuumbwa na kufinyangwa uwe katika sura Yake. Bali kungali kuna ile sifa isiyoweza kuharibiwa. Haiwezi kuharibika kamwe. Ni Mungu, hapo mwanzo. Ni Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu. Na yote ni sifa za Mungu: Uzima wa Milele kwa wana wa wanadamu.

Sasa na tuombe.

Mpenzi Baba wa Mbinguni, tunaomba usiku wa leo ya kwamba Wewe utatubariki na upate utukufu kutokana na kukusanyika kwetu pamoja. Tunaweka wakfu jengo hili na uwanja huu, tukijiweka juu yake na kukupa Wewe, kama toleo, Bwana, kwa ajili ya heshima ya Jina Lako. Tujalie, Bwana. Bariki kila kitu tunachofanya. Jalia kiwe ni cha kumheshimu Yesu Kristo, na kumleta kama kweli iliyo hai miongoni mwa watu.

² Na wakati ibada zitakapokwisha, na tutoke kwenye mikutano hii na kwenda majumbani kwetu, hebu na tuseme kama wale ambao ninii kumi na tisa...miaka iliyopita, Pasaka hii iliyopita, walipokuwa wakitoka Emau, wakati Yeye alipojitokeza miongoni mwao na kufanya jambo lile lile alilofanya kabla ya kusulubiwa Kwake. Yeye alikuwa ni Bwana aliyefufuka, kwa kuwa alikuwa angali anajitambulisha katika mambo yale yale aliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, na macho yao yalifumbuliwa nao wakamtambua. Mungu, jalia tuseme usiku wa leo, baada ya miaka elfu moja mia tisa, tunapokuwa njiani mwetu tukielekea nyumbani, usiku wa leo, jalia tuseme, “Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Jalia ajitambulishe Mwenyewe usiku wa leo, miongoni mwetu, Bwana, kama Bwana aliyefufuka, akiwa tayari kurudi kwa ajili ya Kanisa Lake. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

³ Kila usiku, ili kuweka kitu hicho kwa utaratibu, tunapokuja kuombewa; Ndugu Borders, ama—ama mwanangu, Billy Paulo, mmoja wao, atakuwa hapa kila jioni, kama—kama saa moja kabla ibada hazijaanza. Nao wanaleta kadi ndogo ambazo zina namba juu yake. Mvulana huyu atazichukua kadi hizi na kuzichanganya, moja kwa moja humu ndani, mbele zenu. Mnaona? Kwa hiyo, hilo, ndipo atawapa kadi, yoyote unayotaka. Nitakaposhuka kuja usiku, kila usiku...Hilo linampa mgeni, kila siku, na—nafasi ya kupata kadi ya maombi.

4 Ndipo kila usiku, si wengi mno watakaokuja jukwaani kwa wakati mmoja, bali nitaleta idadi fulani iombewe. Huenda nikaja, nianze kutoka moja pale, ni nne, inaonyesha ya kwamba mvulana anayesambaza kadi hawezi kukuhakikishia jambo lolote, ama kukuuzia kadi ya maombi, ambayo itakuonyesha ya kwamba utaingia kwenye mstari wa maombi. Una nafasi ile ile, kwa sababu kadi huwa zimechanganywa, mbele ya wasikilizaji.

5 Jambo lingine ni, ya kwamba huenda nikaanzia mahali popote. Huenda nikaanza kutoka hamsini, kurudi nyuma kutoka thelathini, kuenda mbele, ama kutoka . . . Ndipo wakati mwingine ninahesabu ni wangapi walio katika safu hii, na kuwagawanya kwa safu hii, na kadhalika namna hiyo, kupata namba fulani. Na wakati mwingine ninamchukua mtoto mdogo, na kuukisia umri wake, ama mwanamume fulani ama mwanamke, ama kitu kama hicho, mwajua, ama chochote kinachoingia moyoni mwangu. Kwa hiyo, hakuna mtu anayejua mahali mstari wa maombi utakapoanzia, na hilo linampa kila mtu fursa. Halafu, mwishowe, sote pamoja, tunamwombea kila mtu aliye na kadi. Kwa hiyo sisi . . . Shikilia tu kadi yako.

6 Sasa mara nyingi, katika mikutano hii, ni kwamba hata watu hawafiki jukwaani. Kama mtu yeyote yupo hapa, ambaye amepata kuwa mkutanoni hapo siku za nyuma; kuna watu kumi wasiopo jukwaani wanaoponywa wakati mtu mmoja anapoponywa jukwaani.

7 Inatakiwa imani. Haidhuru ni wapi, inakubidi ukidhi imani hiyo. Hivyo tu. Na imani si ha—hadithi tu, kitu fulani tu unachowazia. Ni kitu unachojua. Hiyo ni kweli.

8 Na sasa nitawaulizeni, sasa, tunapogeuka sasa tupate kusoma Maandiko, usiku wa leo. Tutasoma kutoka katika Kitabu cha—kutoka katika Kitabu cha Waebrania, usiku wa leo, na sasa wakati tunaposimama kulisoma Neno. Sisi husimama kuonyesha utiifu wetu kwa bendera, na tu—tunasimama kuheshimu nembo zetu zote za taifa, kadhalika, kwa hiyo hebu na tusimame tunapolisoma Neno la Mungu. Sivo? Waebrania, mlango wa 13, kifungu cha 1 hadi cha 8.

Upendano wa ndugu na udumu.

Msisahau kuwafashili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.

Wakumbukeni hao waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao, na hao wanaodhulumiwa, kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili.

Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.

Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.

Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?

Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao.

Yesu Kristo ni yeye yule jana, . . . leo na hata milele.

⁹ Na tuinamishe vichwa vyetu. Bwana Yesu, lifanye hili kuwa halisi kwetu, usiku wa leo. Si kusoma tu kwa Neno, bali jalia Neno lifanyike mwili miongoni mwetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

¹⁰ Tunapozungumza kwa muda mfupi tu, na kila usiku tutajitahidi kutoka ifikapo saa tatu na nusu, kama—kama ikiwezekana. Ninataka kuwashukuru wadhamini wangu, tena, na watu walioturuhusu kupachukua mahali hapa, uwanja huu, wa maonyesho ya mifugo, ama chochote kile. Tunashukuru sana. Sasa, sasa ninyi ni kundi zuri tu la kulizungumzia, nami ningeweza kuzungumza tu kwa muda mrefu, ila sitaki kuwachosha. Kila usiku, kwa kama dakika thelathini; usiku wa leo itakuwa ni muda mrefu zaidi kwa kuwa ndio usiku wa kwanza.

¹¹ Ninataka kuzungumza juu ya somo usiku wa leo la: *Kristo Aliyetambulishwa Katika Nyakati Zote*. Kwa sababu, Biblia inasema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” na utambulisho wa Kristo katika nyakati zote.

¹² Sasa mliona hapa, Maandiko yakisema hapa, ya kwamba, “Wakumbukeni wale wanaowaongoza; mkiuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, mnaona. Mwisho wa mwenendo wao ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹³ Watu wengi sana wana maoni tofauti juu ya Kristo. Ninapopita katika—katika sehemu mbalimbali za nchi, na kote ulimwenguni, ninakuta kwamba watu wengi sana wana maoni yao tofauti. Mngeshangaa kujua kwamba baadhi ya maoni yao ni nini. Baadhi yao wanafikiri ya kwamba Yeye ni mwalimu tu mzuri sana. Vema, sasa, Yeye alikuwa—alikuwa hivyo. Hiyo ni kweli kabisa. Na wengi wanafikiri alikuwa mwanafalsafa mkuu. Ambalo, Yeye alikuwa hivyo. Yeye, hakika, alikuwa hivyo. Na halafu baadhi yao wanafikiri Yeye alikuwa ni mtu m—mzuri. Yeye, Yeye alikuwa hivyo. Lakini, unaona, alikuwa zaidi ya hayo. Yeye alikuwa yote hayo, na zaidi. Baadhi yao wanafikiri ya kwamba Yeye alikuwa ni nabii. Alikuwa ni nabii, bali alikuwa ni zaidi ya nabii. Alikuwa kile manabii walichokuwa, na zaidi. Mnaona? Kwa hiyo, nini, tungejuaaje sasa? Kama

alikuwa akifundisha mafundisho Yake, Yeye alikuwa mwalimu na alikuwa mwanafalsafa mkuu.

¹⁴ Lakini ji—jinsi tu tutakavyopata kujua, leo, kama tulitaka kumtambua, leo, na, ninaamini ya kwamba alifufuka kutoka kwa wafu. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Na ninaamini ya kwamba Yeye ameahidi hapa, ya kwamba, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” “Nami niko pamoja nanyi siku zote, na sitawaacha wala sitawapungukia.”

¹⁵ Sasa, Maneno hayo ni, ama ni ya kweli au si ya kweli. Na kama si ya kweli, basi tunafanya nini hapa usiku wa leo? Sisi ni—sisi ni watu wanyonge, sisi ni watu ambao ni—ambao ni, vema, tumedanganywa; ulimwengu wote wa Ukristo umedanganywa kama Yeye si yeye yule jana, leo, na hata milele, kama Yeye si hai usiku wa leo na hayupo pamoja nasi kama alivyoahidi. “Tazama, niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu, ama mwisho wa dahari. Niko pamoja nanyi siku zote.” Sasa, kama hiyo si Kweli, basi kuna kasoro fulani, nasi—nasi tumekuwa mashahidi wa uongo. Si kwamba tu tunajifanya wenye mashaka, katika ulaghai, bali tunawadanganya wengine. Tumeonekana tu wadanganyifu, wa jambo fulani tunalonena habari zake, jambo ambalo si kweli, kama Yeye ni hadithi tu ama Yeye ni wa kihistoria tu.

¹⁶ Kristo wa kihistoria ana faida gani kama Yeye si yeye yule leo? Mungu wa Musa ana faida gani kama Yeye si—si Mungu yeye yule leo? Inafaa nini kumchukua kurumbizi wa—wako na kumlisha vitamini nzuri, kumfanya awe na manyoya mazuri na mabawa mazuri yenye nguvu, na kisha umweke kwenye kizimba? Unaona, haimsaidii chochote. Nasi tukizungumza jinsi Mungu alivyokuwa mkuu, na kisha tuiseme ni yeye yule leo, basi kuna kasoro fulani. Tumewekwa kwenye kizimba mahali fulani. Na, hilo, hilo ni—hilo ni wazo la uongo la jinsi Mungu alivyo.

¹⁷ Biblia inasema dhahiri, “Ni yeye yule,” na hilo linamaanisha Yeye ni yeye yule. Yuko tu jinsi alivyokuwa. Hajabadilika hata kidogo, na ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁸ Na sasa tunaninii, leo, katika siku hii na wakati huu, kama tu vile walivyofanya katika siku Zake na katika siku zote, tuna wazo letu juu ya jambo Hilo. Lakini, hakika, kama kuna njia yoyote ulimwenguni ambayo tungejua hakika, itatubidi kutafuta kujua kile Yeye alichokuwa, na halafu tutafute kujua jinsi alivyokuwa katika nyakati zingine.

¹⁹ Kumbukeni, Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kwa hiyo inatubidi kutafuta kujua jinsi alivyo, kutoka kwenye nyakati zingine; kujua jinsi alivyokuwa katika wakati alipotembea duniani, ule wakati kabla hajatembea duniani, na ule wakati baada ya Yeye kuwako duniani na kuondoka duniani. Itatubidi kutafuta kujua jinsi alivyokuwa, tupate kujua jinsi alivyo leo, daima, maana Yeye ni yeye yule jana, leo, na

hata milele. Sasa, lakini, vinginevyo, itatubidi kurudi nyuma na kutafuta, tuone chochote alichokuwa.

²⁰ Sasa tunaona, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 1, kuanzia kifungu cha 1, inasema, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu.” Sasa hizo ni sifa, Maneno Yake; hayo ni mawazo sasa, hayajathamkwa. Unaona, “Hapo mwanzo ni, kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Hapo mwanzo kulikuwako Neno!” Vema, kama Yeye alikuwa Neno hapo mwanzo, Yeye ni Neno leo, kwa maana Yeye daima ni Neno.

Sasa Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kitu fulani.

²¹ Nao watu wanasema, vema, sasa kama... Kama ningemwuliza Mkatoliki hapa usiku wa leo, je! unafikiri Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kitu gani? Mkatoliki angesema, “Kwa kanisa Katoliki.” Vema, sasa ni kanisa Katoliki lipi? Sasa wana la Kirumi, la Kiorthodoksi ya Kiyunani, na mengi yao. Ingekuwa ni kanisa lipi la Kikatoliki? Walutheri wanasema, “Kwa sisi,” basi ninyi Wabaptisti mko nje. Halafu basi kama tungenesema, “Kwa la Kibaptisti,” basi ninyi Wapentekoste mko nje. Kwa hiyo kungekuwako na mchafuko kwelikweli, hakuna mtu angalijua la kufanya, kwa hiyo Yeye kamwe hakuahidi kuuhukumu ulimwengu kwa kanisa.

²² Yeye aliahidi kuuhukumu ulimwengu kwa Kristo, Naye Kristo ni Neno. Na Biblia ndiyo itakayouhukumu ulimwengu, ambayo ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

²³ Sasa, kama Yeye alikuwako hapo mwanzo, Yeye aliligawa Neno Lake, kiasi fulani, kwa kila kizazi, kila wakati ambapo Yeye—ambapo alikuwa na wakati huu unaokuja.

²⁴ Yeye yupo kila mahali, anajua yote, ana nguvu zote, na hana kikomo. Kama sivyo alivyo, Yeye si Mungu. Akiwa asiye na kikomo, Yeye ni—Yeye ni—Yeye ni wa Milele. Na halafu basi, katika jambo hilo, akiwa yupo kila mahali; akiwa anajua yote, akijua mambo yote, linamfanya aliye kila mahali. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

²⁵ Kwa hiyo, basi, Yeye angeweza kujua mwisho kutoka mwanzo, na katika kila wakati Yeye aligawa kiasi fulani cha Neno Lake, katika kila wakati.

²⁶ Halafu basi, kwa kawaida, mwanadamu analivuruga sana, na ulimwengu unakuwa katika hali mbaya sana, mpaka inambidi kumtuma mtu fulani, aliyetiwa mafuta. Nyakati zote zimekuwa vivyo hivyo. Yeye hujitambulisha juu ya nchi, katika mwanadamu. Mungu hafanyi kitu bila mwanadamu. Biblia ilisema hivyo, mwajua. Unaona? Yeye daima humchukua mwanadamu, maana ilimbidi kumtumia mwanadamu, na kumwacha mtu huyo... Akamweka awe

na uhuru wa kujichagulia, akijua ya kwamba angeanguka, kusudi apate kuonyesha sifa Zake kama Mwokozi, kwa maana hakukuwako na kitu chochote kilichopotea. Na, kwa hiyo, Yeye alimchagua mwanadamu. Angaliweza kuchagua nyota, angaliweza kuchagua miti, bali Yeye alimchagua mwanadamu.

²⁷ Wakati mmoja, akisimama, akiangalia mavuno; Yesu, Yeye alisema, “Mavuno yameiva. Wafanyakazi ni wachache. Mwombeni Bwana wa mavuno atume wafanyakazi katika mavuno Yake.” Naye alikuwa ndiye Bwana wa mavuno. Mnaona? “Hamna kwa maana hamwombi. Hamwombi kwa maana hamwamini. Ombeni kwa wingi, furaha yenu iwe timilifu.” Mnaona? Yeye anawatarajia mwombe, na kuamini ya kwamba mnapokea mnachoomba.

²⁸ Sasa, basi, hapo mwanzo, tunaona ya kwamba Yeye aliligawa Neno Lake. Tunaona, katika siku za Musa na kote kote katika siku za nyuma, ya kwamba Yeye—Yeye anajitambulisha Mwenyewe kila wakati kwa manabii Wake. Biblia inasema, “Yeye hafanyi neno mpaka kwanza awafunulie manabii Wake.” Na, kumbukeni, Mungu ni Mungu asiyebadilika. Kamwe habadiliki. Yeye hudumu yeye yule jana, leo, na hata milele.

²⁹ Sasa tunaona, katika kila wakati, ya kwamba mwanadamu huingilia mpango wa Mungu. Wanawazia kwa akili zao wenyewe, na linaonekana ni zuri. Linaonekana ni zuri, zuri sana. Na wakati mwingine linafanana sana huenda kukawa na tofauti ya neno moja, bali neno hilo moja linamaanisha tofauti kati ya mauti na Uzima.

³⁰ Neno moja ndilo lililosababisha mambo kuanza, wakati Hawa alipoacha kusadiki sehemu moja ya Neno la Mungu. Kumbukeni, yeye hakuninii... Shetani kwa namna fulani hakulitupilia tu lote nje. Yeye alisema, “Loo, hakika Hili litakuwa hivi, na Hili litakuwa vile, na Mungu ninii, lakini hakika Yeye hatafanya jambo *hili*.”

³¹ Bali Yeye alisema angelilifanya, na, wakati aliposema angelilifanya, hilo linakuwa hivyo. Mnaona? Ninii tu, lazima uamini kila sehemu Yake. Haidhuru linasema nini, liamini hata hivyo. Kama huwezi kulielezea, liamini hata hivyo. Huwezi kumleleza Mungu; hakuna mtu anayeweza. Mungu anajulikana kwa imani, sio kwa sayansi. Unamwamini Mungu kwa imani, kwa sababu Yeye alisema hivyo, na hilo latosha. Mradi tu alisema ndivyo, hilo linatibu kisa hicho. Yeye alisema hivyo; haileti tofauti yoyote kiasi gani sayansi inasema siyo lilivyo.

³² Nuhu, Nuhu asingeweza kuelezea jinsi maji yalivyokuwa huko juu mbinguni, sababu sayansi ilisema hayakuwako. Bali kama Mungu alisema hivyo, Yeye anaweza kuweka maji huko juu, kwa hiyo hilo—hilo lilitosha. Unaona, yeye alimwamini Mungu tu.

³³ Daima, mtu ambaye ametiwa mafuta na Neno, anasadiki yale Mungu aliyosema. Haidhuru kama Yeye anaweza kuthibitisha jambo hilo, ama hawezi, analiamini haidhuru. Mungu Ndiye anayethibitisha.

³⁴ Sikilizeni, leo sisi siku zote ni kama...Mwanadamu siku zote anamsifu Mungu kwa yale aliyokwisha kufanya, wakati wote anatazamia yale atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya. Daima limekuwa ni jambo lile lile. Na kila mtu ana tafsiri yake mwenyewe binafsi.

³⁵ Mungu ndiye anayejifasiria. Mungu hahitaji mtu yeyote kufasiri. Biblia ilisema si la kufasiriwa. Haihitaji mwanadamu. Mungu huifasiri Biblia, Yeye Mwenyewe. Mungu alisema, "Iwe nuru," na ikawa nuru. Hilo latosha. Mungu alisema, "Bikira atachukua mimba," naye akachukua. Hilo lilitosha. Mungu anaposema jambo lolote, na kulithibitisha, hiyo ndiyo fasiri Yake ya jambo hilo. Yeye alisema ange- "mwaga Roho Wake" katika siku hizi za mwisho, Naye alifanya hivyo. Hakuna fasiri yake; tayari limefasiriwa. Wasioamini huenda wakainuka, na wenye kushuku huenda wakasimama, na lolote wangeweza kufanya; bali Mungu alifanya jambo hilo, hata hivyo, kwa sababu Yeye alisema angefanya hilo. Hahitaji mtu yeyote kumfasiri. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Aliweka ahadi, watu wanaiamini, Naye anawafasiria hiyo.

³⁶ Yeye ni Bwana anayeponya magonjwa yetu yote. Siwezi kuwaambia jinsi anavyofanya hilo, bali analifanya. Yeye alisema angelilifanya, ya kwamba angelilifanya, kwa hiyo ni juu ya imani yetu. Asingeweza kulifanya kule bila imani, wala hawezi kulifanya hapa, ama wakati wowote, bila imani.

Sasa, Yeye ni Neno. Yeye ni Neno lililotambulishwa kwa ajili ya wakati huo.

³⁷ Sasa, shida ya watu, siku hizi, tunawakuta wakiishi katika nuru ya wakati mwingine. Kama tu vile Yesu alivyokuta wakati alipokuja, Yeye aliwakuta wakiishi katika nuru ya torati, na wakipuuza kile kilichokuwa kitukie katika wakati Wake. Mnajua shida ya siku hizi ni nini? Kuna shida gani na ninii . . .

³⁸ Walutheri walikuwa na shida gani? Vema, kwa sababu walikuwa wakiishi katika mwangaza wa wakati wa Kilutheri, wakati John Wesley alipopata siri ya utakaso. Wasingeweza kusonga mbele, kwa kuwa walikuwa wakiishi katika mng'ao wa wakati wa Luther.

Ilikuwa je kwa Wapentekoste?

³⁹ Mbona, Wesley alikuwa amejiundia madhehebu sana, mpaka alikuwa akiishi katika mwangaza wa wakati mwingine, walikuwa kwenye wakati wa Wesley, wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu ulipowashukia Wapentekoste. Unaona, walikuwa wakiishi katika yale Wesley aliyosema, utakaso. Ilikuwa ni vigumu kwao kuamini ubatizo wa Roho Mtakatifu, kule

kurudishwa kwa karama. Walikuwa wakiishi katika nuru ya wakati mwingine.

⁴⁰ Na hivyo ndivyo walivyokuwa wakifanya wakati Yesu alipokuja. Kasema, “Tunaye Musa. Sisi, tunaye Musa.”

⁴¹ Yeye akasema, “Kama mngalimjua Musa, mngalinijua na Mimi. Musa aliandika habari Zangu. Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Hayo ndiyo Maandiko yaliyopaswa kuwa.

⁴² Mungu akijitambulisha, akiyafasiri Maandiko Yake kwa wakati ule, na daima ni Kristo. Ni Kristo katika kila wakati. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Daima imekuwa ni Kristo.

⁴³ Sasa tunaona, ya kwamba sasa tunawaona ndugu zetu Wapentekoste wanaishi katika nuru ya wakati wa Kipentekoste, nao bado wangali wanalikosa jambo Hilo. Wanajaribu kuufasiri wakati wa Kipentekoste, wakati tumeupita huo kwa mbali. Tunaishi karibu na wakati wa kunyakuliwa, kwa kule kuja kwa wa—wakati wa mwisho. Bali hivyo ndivyo mwanadamu anavyofanya, ndivyo ilivyo tu.

⁴⁴ Tuna kiasi fulani ambacho kimepangiwa kila wakati. Biblia imegawanywa hivyo, na hivyo ndivyo inavyotupasa kuwa nayo. Haina budi kuwa hivyo.

⁴⁵ Mungu asiyebadilika, akiwa na tabia isiyobadilika, na tabia Zake zinabaki tu vile vile. Yeye hawezi kubadilisha tabia Yake. Hawezi kufanya hivyo. Kitu chochote hutambulikana kwa tabia yake.

⁴⁶ Sijui kama ninyi nyote mna nyundomanjano huku ama hamna, kungurumilia...tunawaita nene, na nde—ndege anayeitwa kungurumilia. Wote ni saizi moja. Ukimwangelia kungurumilia akiruka, kama yuko umbali fulani na umwangelie, yeye atafanya mstari wa B wakati anaporuka. Lakini, nyundomanjano, yeye atapanda na kushuka anaporuka. Unaona, hiyo ndiyo tabia ya nyundomanjano. Unaweza kumtambua kwa matendo yake.

Mwangelie mtu akitumia mkono wake wa kulia ama wa kushoto. Yeye ni m- . . .

⁴⁷ Tuna wanawake siku hizi wanaotaka kuwa wanaume. Wanavaa kama wao, bali wangali...Waangelie wakitembea na kile wanachofanya, wangali...Tabia yao inaonyesha ya kwamba wao ni wanawake, hata hivyo, vile vile tu, unaona, kwa maana ni jinsi hiyo tu. Tutafikia jambo hilo baadaye. Lakini, hata hivyo, tuko kwenye jambo jingine sasa hivi.

Kumbuka, unatambulishwa kwa tabia.

⁴⁸ Na Mungu hutambulikana kwa tabia Yake iliyo kuu, ya kwamba, “Yeye hawezi kubadilika.” Yeye alisema, katika Malaki

3:6, “Mimi ni Mungu, wala sibatiliki.” Mnaona? Yeye habadiliki yakini. Tabia Zake ni zile zile.

⁴⁹ Kila wakati alipojitokeza duniani, katika mwisho wa wakati, Yeye siku zote alimtuma mtu na akamtia mafuta kwa Roho Mtakatifu, Kristo. Roho Mtakatifu ni Kristo, “aliyetiwa mafuta,” yule *Logos*, naye alitoka, naye anakuja kutambulisha Ma—Maneno ya wakati huo. “Neno la Bwana huwajia manabii,” Biblia ilisema hivyo, na anautambulisha wakati huo. Unaona, Yeye hafanyi lolote nje ya mwanadamu. Sasa Yeye hawezi kufanya hivyo katika kundi. Huwezi kufanya jambo hilo. Halijapata kufanywa kabisa. Yeye kamwe hajawahi kutumia kundi; hajawahi kamwe. Yeye humtumia mtu mmoja peke yake. Wewe si ninii. . .

⁵⁰ Israeli waliokolewa kama taifa, ila wewe utaokolewa kama mtu binafsi.

⁵¹ Naye humtumia mtu mmoja. Yeye alikuwa na...Hata hakuwa na Mu—Mu—Musa na Eliya, wakati ule ule. Asingeweza kuwa na Eliya na Elias, wakati ule ule. Asingeweza kuwa na Yohana na Yesu, wakati ule ule. Yeye daima ana mmoja, kwa sababu Yeye humchukua mtu huyo mmoja akamwingiza katika mapenzi Yake ya Kiungu.

⁵² Kama tulianza usiku wa leo, nami nikamchukua mtu mmoja, mtu fulani hapa ambaye ningemchagua, na tungekubaliana katika mafundisho, kikamilifu kabisa, tungeanzisha kundi dogo. Katika mwaka mmoja tangu leo, tungekuwa na akina Ricky wengi sana mle ndani, mbona, ingekuwa ni aibu. Hiyo ni kweli, wanaingia tu kama kupe. Huwezi kuwazuilia nje. Hivyo, basi, kamwe haukuwa ni mfumo wa Mungu.

⁵³ Mungu hawezi kubadilika. Yeye hushughulikia, vivyo hivyo, mtu mmoja binafsi! Alifanya hivyo kote katika nyakati. Yeye siku zote amefanya jambo hilo.

⁵⁴ Na tabia yake hutambulishwa kwa wakati huo. Sasa, msisahau jambo hilo, tabia Yake hutambulishwa katika wakati huo.

⁵⁵ Angalia katika siku za Yusufu, yule nabii, jinsi ambavyo Yesu alitambulishwa kikamilifu katika Yusufu. Yeye alizaliwa, akapendwa na baba yake, akachukiwa na ndugu zake, bila sababu. Yeye aliwapenda ndugu zake. Bali walikuwa Mafarisayo waliojipiga msasa, tuseme, wala hawakuwa na uhusiano wowote naye, nao walimchukua kwa sababu aliona maono na—na kadhalika. Lakini tabia yenyewe iliyokuwa ndani yake ilionyesha ya kwamba ilikuwa ni Kristo.

⁵⁶ Yusufu alikuwa ni nabii. Alitabiri mambo. Yalitukia sawasawa kabisa tu jinsi yalivyotukia. Jinsi alivyoyanena, hivyo ndivyo yalivyotukia. Naye alifasiri ndoto, wala yeye kamwe hakutoa tafsiri iliyo mbali sana. Kila wakati aliposema ingekuwa hivyo, hivyo tu ndivyo ilivyokuwa. Yeye alizaliwa,

nabii, kwa ajili ya wakati ule. Kweli kabisa. Sasa, tunaona ya kwamba Mungu alionyesha tabia Yake katika Yusufu.

⁵⁷ Kila mmoja wa manabii alionyesha tabia ya Mungu, kwa kuwa walichukua Neno la wakati huo na kulitambulisha. Mungu alifasiri Neno Lake, la wakati huo, kupitia mtu huyo. Sasa, hakuna mtu yeyote anayeweza kupata kosa katika jambo hilo. Hayo ni Maandiko.

⁵⁸ Vema, kama daima imekuwa hivyo, hivi haitaibidi kuwa vivyo hivyo leo, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele! [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

⁵⁹ Mungu alifasiri Neno Lake Mwenyewe! Yeye alisema, “Jambo *hili* litatukia katika wakati fulani, na *hili* litatukia,” Naye anashuka na kulifanya. Sasa, Yeye hahitaji kufasiriwa kokote kwake, maana linajifasiri lenyewe. Yeye hahitaji mtu yeyote kumfasiri. Yeye ni Elohimu, anayeishi peke yake, anayejitosheleza kwa yote. Yeye hahitaji msaada wowote kutoka kwa mtu yeyote. Mnaona, Yeye ni Mungu, Naye hufanya anavyotaka.

⁶⁰ Na kuna jambo moja ambalo tuna hakika ya kwamba Yeye hawezi kulifanya; Yeye hawezi kulipinga Neno Lake, na kisha abaki kuwa Mungu. Inambidi kulitunza Neno Lake, kwa maana Neno ni Mungu. Ni...Naye Mungu hujitambulisha kupitia kwenye Neno Lake lililoahidiwa kwenye wakati fulani.

⁶¹ Katika ninii fulani, katika siku za nanii, sasa ninii, katika siku za Musa? Yeye alitambulishwa. Alitambulishwa kwa sababu Yeye alitambulishwa na Neno Lake. Alimwambia Ibrahimu, “Uzao wako utakuwa mgeni katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne. Nitawatoa kwa mkono wenye nguvu.”

⁶² Sasa, wakati hii ishara kuu mno ilipotukia, kama donge kubwa la Moto katika kijiti kilichowaka moto. Musa alikuwa ni mkemia. Alikuwa amefundishwa katika hekima yote ya Wamisri. Vipi kama Musa angalitegemea msimamo wa elimu yake, na kusema, “Hebu angalia ule mti wa kuchekeka! Unawaka moto. Unaungua. Majani yake yanazibuka, wala hakuna kitu kinachoangamizwa, kinachoteketea. Sasa, kile kikiisha kuteketea, nitachuma baadhi ya majani nishuke niende kwenye maabara nichunguze yamenyunyiziwa kemikali ya aina gani”? Isingelizungumza naye kamwe! Bali wakati alipotoa viatu vyake, akatembea kwa unyenyekevu!

⁶³ Hivyo ndivyo tunavyompata Mungu, tunapoondoa majivuno yetu na kuyaweka chini, na kuingia katika ule Uwepo.

⁶⁴ Sikilizeni sauti hiyo ikitambulisha. “MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Ninakumbuka ahadi Yangu, na ninaona hali iko sawa. Nimeshuka, nami nitanena. Nami ninakutuma, nawe utakuwa sauti Yangu.” Loo, jamani!

⁶⁵ Hivyo ndivyo Yeye anavyofanya jambo hilo. Yeye alifanya jambo hilo vipi? Kwa kujitambulisha Mwenyewe katika tabia Yake, katika mambo ya kimbinguni. Mambo ya kimbinguni mara nyingi ni ya ajabu sana, yanawapita watu kwa mbali. Watu wanakuwa ni watu wazuri, watu waungwana, lakini mara nyingi wanaelewa vibaya.

⁶⁶ Hivyo ndivyo, hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Yusufu. Hakuweza kufahamu. Yeye ni mwana wa Daudi, bali hakuweza kufahamu jinsi ambavyo Mariamu angeweza kupata mimba. Sasa, hapana shaka, akiwa na hayo macho makubwa, mazuri ya hudhurungi, alimwangukia usoni, na kusema, “Mpenzi, ninajua tumefanya nadhiri ya kufunga ndoa. Nina jambo fulani la kukwambia. Nimezuriwa, na Gabrieli, nami ni... nimepata mimba, ‘ya Roho Mtakatifu,’ Yeye aliniambia. ‘Na kitu hiki kitakachozaliwa hakitakuwa mwanao; kitakuwa ni Mwana wa Mungu.’” Na, sasa, Yusufu alitaka kuamini jambo hilo. Bali a—asingeliamini hata kidogo, ilikuwa ni vigumu. Lilikuwa ni jambo gumu sana kwake kuamini. Lakini, mwajua, lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida. Wanawake hawakupata mimba, wakiwa ni bikira, kwa hiyo lilikuwa lisilo la kawaida.

⁶⁷ Na hayo ndiyo mambo yasiyo ya kawaida ambayo Mungu anafanya. Yanawakwaza watu. Yanaangazia, yanayafungua macho ya wengine, na kupofusha wengine, wakati uo huo. Yalifanya hivyo daima, Yeye—Yeye, mambo yasiyo ya kawaida na njia isiyo ya kawaida.

⁶⁸ Laiti Yusufu angalianguka katika Maandiko, apate kuona kile kilichokuwa kitukie katika siku hiyo. Sasa, hakukuwako na manabii wakati huo. Hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne. Malaki alikuwa ndiye nabii wao wa mwisho. Na manabii walikuwa ni watu wasio wa kawaida sana. Kwa hiyo hawakuwa na manabii katika siku hizo, kwa hiyo Mungu alichukua njia ya pili, na kumpa ndoto, na kumwambia. “Yusufu, ewe mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu mkeo, kwa maana mimba yake, ndani yake, ni ya Roho Mtakatifu.”

⁶⁹ Unaona, Mungu akijitambulisha Mwenyewe, Yeye hufanya hivyo daima katika namna za kimbinguni.

⁷⁰ Sasa, hawa, Yusufu na Musa, na kama tungalikuwa na wakati mwingi tungeweza kuendelea na kuendelea tu na jambo hilo. Bali mnafahamu ninalomaanisha, ya kwamba, Mungu, katika kila wakati, daima humtuma mtu binafsi, mtu mmoja.

⁷¹ Kwa hiyo kwa nini unajining'iniza kwenye kundi fulani, wakati wao wako makosani kabisa? Biblia ilisema hivyo, Ufunuo 17, wote watakusanywa katika kundi moja kubwa. Bali kutoka mle watatokea watu mmoja mmoja walio wanyofu kwa Mungu, si hilo kundi lililo sahihi; mtu binafsi ndiye aliye sahihi, mtu mmoja mmoja katika hilo kundi. Sasa tunaona, basi, tunazozana

na kuendelea, kuhusu, “Sisi ni wafuasi wa *hili*, na ni wafuasi wa *lile*.” Hilo halimaanishi chochote kwa Mungu.

⁷² Ni wewe kama mtu binafsi, mbele za Mungu. Kama... Inakubidi usimame kwa miguu yako mwenyewe. Wewe ndiwe unayepaswa kutoa ushuhuda. Kila mmoja wenu hana budi kufanya jambo hilo, kuwajibika kwa Mungu kwa ajili ya Ufunuo.

⁷³ Sasa vipi kama ninazungumza hapa na mtu ambaye kwa kweli hawezi kulipokea, hamna kitu ndani yake cha kupokelea? Biblia ilisema, “Yeye anayeishi katika anasa amekufa yungali hai.” Kwa nini hao Mafarisayo hawakuliona?

⁷⁴ Mwangelie Yesu, yote tuliyojua, Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Tunaamini jambo hilo. Biblia ilisema ilikuwa hivyo. Vema, angalia wakati alipofanya ishara yake ya Kimasihi.

⁷⁵ Mafarisayo, waliokuwa na nuru kidogo. Walikuwa ni watu wazuri, waliishi maisha mazuri ya Kikristo, ama maisha mazuri ya kidini, walikuwa na nuru kidogo maishani mwao. Walikuwa na madhe... waliunda madhehebu, na ukuhani. Walikuwa na nuru kidogo. Lakini chini katika moyo wao, hawakuwa na uwakilisho wa Milele Utukufuni. Kwa hiyo wakati walipoona mambo ya kimbinguni yakifanywa, wao walisema, “Mtu huyu ni Beelizebuli, ibilisi.” Na ni jambo gani lililotukia? Hilo lilizima nuru waliyokuwa nayo.

⁷⁶ Lakini hapa palikuwa na maskini mwanamke, mwenye sifa mbaya, kahaba. Ndani ya moyo wake, vema, yeye alikuwa na uwakilisho wa moja ya mawazo ya Mungu. Huyu hapo, amelemewa na dhambi. Bali wakati alipoona jambo hilo likitukia, yeye alisema, “Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni nabii. Ninajua wakati Masihi atakapokuja Yeye atatwambia mambo haya.” Ilifanya nini? Iliyafisha maisha yake. Yeye alikuwa ni Mkombozi, kwake, kwa kuwa Yeye aliweza kumwinua mahali alipotoka.

⁷⁷ Lakini Farisayo huyu, wazieni jambo hilo, akiwa wa kidini alivyoweza kuwa, na Yesu alisema, “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mtazifanya.” Watu wa kidini, walikuwa ni wafuasi wa mashirika mazuri, ya matabaka ya juu. Naye Yesu aliwaita, “Waovu, na ibilisi.” Waliikataa nuru ya saa. Hivyo ndivyo ilivyo hasa.

⁷⁸ Yesu katika wakati Wake, je! Yeye alikuwa ni nani? Ni kama tu manabii wa wakati wao, kila mmoja wao alikuwa ni Neno la Mungu likifasiriwa kwa ajili ya wakati huo.

⁷⁹ Musa alikuwa ni Neno la Mungu, lililofasiriwa. Mungu alisema, “Nitatuma huko, nami nitawakomboa. Ninakutuma huko na Neno Langu. Nitafanya ishara kuu na maajabu.” Yeye alifanya hivyo.

⁸⁰ Mariamu, yeye alikuwa Neno la Mungu, lililofasiriwa. “Bikira atachukua mimba.” Hilo lilikuwa ni Neno la Mungu, lililofasiriwa.

⁸¹ Sasa huyu hapa Yesu anajitokeza, Mungu wa manabii. Nao walikuwa ndio hawa hapa, wameunda madhehebu kweli kweli na wamepotoka, na, loo, katika hali ambayo hata wasingeweza... Hata hawakumtambua. Yeye kamwe hakuja jinsi walivyodhani anapaswa kuja. Walidhani Mungu angevuta wenzo mdogo *hapa*, na kushusha ushoroba wa Mbinguni, Naye angetembea na kusema, ‘Kayafa, kuhani mkuu wa Mungu, nimewasili.’”

⁸² Lakini alikuwa na mtoto aliyezaliwa katika hori, huko chini katika pango do—dogo, hori la g’ombe huko Bethlehemu. Huko chini kabisa, kukiwa na nyasi kavu na samadi ya banda, mtoto mchanga aliyefungwa kwa nguo za kitoto, na akalazwa horini. Hakuwa na elimu. Angalieni jinsi walivyolisahihisha Neno? Kwa kuwa, Yeye alikuwa ni Neno. Yeye ni Neno. Yeye anadumu vivyo hivyo yeye yule, jana, leo, na hata milele. Kweli.

⁸³ Sasa, mimi sifanyi ninii yoyote, sisukumii chochote, kwa mtu yeyote ama kitu chochote. Hilo silo kusudi langu kufanya jambo hilo. Kama hilo lingalikuwa moyoni mwangu, ningalienda mbele ya madhabahu hii, na kutengeneza mambo, kwanza.

⁸⁴ Lakini, angalieni, kwenu ninyi watu mnaomwomba Mariamu, kama mpatanishi; hebu mwangalieni Mariamu. Ninaamini yeye alikuwa ni mwanamke bikira, hakika, bali alikuwa ni kiangulio tu ambacho Mungu alitumia kumleta Kristo duniani. Nyumba ambayo...

⁸⁵ Mungu alitanua hema Lake, kutoka kuwa Yehova, akawa mtu. Alikuwa ni *Imanueli*, “Mungu akiishi pamoja nasi,” akipiga kambi pamoja nasi; Mungu, aliyeshikwa katika mwili; Mungu, aliyefanyiwa makao katika hema iliyoitwa mtu, huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

⁸⁶ Mwangalieni Mariamu. Huyu hapa Mvulana, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, kamwe hajawahi kwenda shule hata siku moja, tujuavyo sisi; huyu hapa, amesimama hekaluni, akihojiana na makuhani. Pia angalia, huyu hapa baba na mama wanakuja, siku tatu usiku na mchana, walikuwa wamempoteza, nao wakampata hekaluni. Wakasema, “Mwanangu, tumekutafuta...” Mariamu, hebu msikilizeni Mariamu, akasema, “Sisi, mimi na baba yako tumekutafuta, mchana na usiku, kwa machozi.” Angalieni hapo, akikana ushuhuda wake. Alimwambia Yusufu ya kwamba Roho Mtakatifu alimtia uvuli; aliwaambia hao makuhani ya kwamba Huyu alikuwa ni mtoto aliyezaliwa kibikira; naye huyu hapa amesimama, na kusema, “Baba Yako, Yusufu, pamoja na mimi.” Mnaona jinsi hilo lisivyo sahihi?

⁸⁷ Bali angalia Neno la Mungu, lilisema, “Hamjui kwamba inanipasa kuwa katika shughuli za Baba Yangu?” Neno daima husahihisha kosa kwa kumtambulisha Mungu miongoni mwao. Mtoto mwenye umri wa miaka kumi na miwili, kama angalikuwa, Yusufu angalikuwa baba Yake, angalikuwa akijenga nyumba na makabati. Bali alikuwa huko nje akiyararua hayo madhehebu ya siku hiyo. Alikuwa akifanya kazi ya Baba Yake. Unaona yale aliyokuwa akifanya? “Na hamjui ya kwamba inanipasa kuwa katika shughuli za Baba Yangu?” Unaona, alimwambia mama Yake, mnaona jinsi hilo...? Vema, Yeye alikuwa ni lile Neno.

⁸⁸ Yeye ni Neno, nalo Neno husahihisha kosa kwa kutambulisha sifa ya Mungu. Amina. Angalia, wakati ulimwengu...

⁸⁹ Ninaweza kumwazia Simoni Petro. Nilisoma hadithi fupi wakati mmoja, juu yake na—na ndugu yake, Andrea. Na jina lake lilikuwa ni Simoni wakati huo, mwajua, wala hakuwa ameitwa Petro bado. Kwa hiyo yeye na ndugu yake walikuwa ni wavuvi, pamoja na baba yao, nao walikuwa huko baharini. Naye mzee huyo alikuwa akizeeka, ndipo akawaita kwenye kile chombo, usiku mmoja, na kusema, “Enyi wavulana, mnajua ya kwamba tumemtumaini Mungu. Mara nyingi tumekuwa hatuna kitu cha kula, na tulikuwa na madeni ya kulipa. Na—nasi tungetoka tukaenda, bila kuvua samaki, kwa siku mbili tatu. Nami pamoja na mama yenu, mbele zenu... aliondoka, mbona, sote tungekusanyika na kuomba, naye Mungu angetupa samaki wengi. Enyi wavulana, nimentumaini Mungu, maishani mwangu mwote. Nami daima niliishi kama Mwebrania yeyote mnyofu, kumtarajia Masihi kuja. Sasa, enyi wavulana, ni—ninazeeka mno sasa. Labda sitamwona, lakini ninataka ninyi wavulana mfunzwe vizuri.”

⁹⁰ Ninaweza kumwona akimkumbatia Simoni, na mkono mmoja ukimkumbatia Andrea, na kusema, “Enyi wavulana, kabla tu ya kuja Kwake, mtaona mlipuko. Kutakuwako na kila namna ya vitu vya uongo vitakavyoinuka, kwa hiyo vitayapofusha tu macho ya watu.” Daima huyapofusha; na viliyapofusha tu. “Kutakuwako na kila namna ya... Lakini, kumbukeni, msidanganyike. Masihi atakuwa ni nabii. Maana, Musa alisema, katika Kumbukumbu la Torati mlango wa 18, kifungu cha 15, ‘Bwana Mungu wenu atamwinua Nabii mithili yangu.’ Sasa, hatuna manabii wowote wa kudhihirisha Neno la Mungu. Hakukuwako na wowote hapa wa kujiliwa na Neno, kwa hiyo tumekuwa tu na mambo ya kimadhehebu kwa mamia na mamia ya miaka. Lakini wakati Yule atakapowasili jukwaani, msidanganyike, Yeye atakuwa ni nabii. Bwana atajitambulisha Mwenyewe. Yeye atakuwa ni nabii. Na, wakati atakapokuja, Yeye atajitambulisha kama nabii.”

⁹¹ Ninaweza kuwazia siku moja ambayo Simoni alikuwa akishuka kwenda kumwona Yesu pale ufukoni. Na wakati alipoenda Mbele za Yesu, Yesu alimwanguka na kusema . . .

⁹² Alikuwa ndiyo kwanza tu aanze huduma Yake, sasa, Yohana Mtakatifu mlango wa 1, na baada ya “Neno kufanyika mwili na kukaa kwetu,” Huyu hapa. Sasa, tunaambiwa ya kwamba Andrea alimwona Yeye wa kwanza, na akamsikia Yohana akihubiri, na akajaribu kumshawishi Simoni aende. Naye akaninii tu, “Loo, vema, ni mhubiri mwingine tu. Achaneni nao. Na kumekuwa na *hiki, kile*, ama *kinginecho*.” Lakini, muda si muda mnajua, walidhani wanguka waone.

⁹³ Yeye alisema, “Sasa Masihi amewasili!” Loo, Andre . . . Simoni asingeweza kuamini jambo hilo.

⁹⁴ Kwa hiyo alitembea tu siku moja akafika mahali Yesu alipokuwa amesimama. Yesu alikuwa amesimama huko chini ziwani asubuhi hiyo, nao watu wote walikuwa wamekusanyika. Nao wanawake wakaosha vyombo upesi sana, kisha wakaweka nguo zao kando, na kila kitu ambacho wasingeosha siku hiyo, wakashuka wakaja kumsikiliza akizungumza. Simoni alikuwa amevua usiku kucha kule, na labda hakuwa ameshika samaki yeyote wala chochote kile. Akatoka akaenda, akawaza, “Nadhani nitasikiliza tu yale Yeye asemayo.” Akamwendea.

⁹⁵ Yeye alikuwa Jamaa aliyeonekana wa kipekee. Biblia ilisema, “Hana uzuri hata tumtamani.” Hakuonekana kama mfalme.

⁹⁶ Uzuri ni wa ibilisi, siku zote. Hiyo ni kweli kabisa. Na huenda tukafikia jambo hilo, muda kidogo baadaye, ili kwamba basi tuone. Tunaona kile Kaini alichotoa sadaka, na tunaona jinsi ilivyokuwa Mbinguni, na tuone kile ulimwengu huu, urembo wa bure ni nini, na ni kitu gani. Hollywood imechukua uongozi, leo, hata kanisa. Naam, bwana. Ni dhana ya uongo, ya ibilisi.

⁹⁷ Katikati ya uzuri wa Bwana, katika utakatifu na Nguvu; si katika rangi, na poda, na kaptura, na chochote kile wanachojitahidi sana kuvaa na kufanya. Ni katika uzuri wa utakatifu na haki. Sisi si wa ulimwengu huu. Tumetoka katika ufalme ulio huko Juu, ambako haki inadumu ndani yake. Naam.

⁹⁸ Hawatajipamba na Hivyo. Televisheni nyingi mno, na kadhalika.

⁹⁹ Kwa hiyo tunaona ya kwamba Simoni alienda Mbele Zake, na pale alisimama Yule ambaye Andrea aliamini alikuwa ni Masihi. Na wakati Yesu, mara tu alipomwanguka Si—Simoni, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Alijua basi kwamba Huyu alikuwa ni nani. Hakuwa na dhahaka ya kwamba huyo hapo alikuwa ni Mungu aliyetambulishwa tena papa hapa katika Maandiko, tabia Yake ile ile.

Laiti Yusufu angaliweza tu kuangalia nyuma kule na kuona jambo hilo!

¹⁰⁰ Yesu, alipokuwa akihubiri hapa duniani, Yeye alisema... Yeye alisema, “Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele; Hayo ndiyo yanayonishuhudia.” Laiti wangeliondoa macho yao kwenye torati. Torati ilikuwa ni ya tangu siku hiyo, nao walikuwa wakiishi katika mng’ao wa namna hiyo. Lakini ndio hawa hapa leo, wasingeweza kuona Maandiko yakitambulishwa papo hapo. Nao walishindwa kuona Hilo.

¹⁰¹ Nao wamefanya jambo hilo katika kila wakati, nao watafanya hilo katika huu, pia. Hakuna kitu kingine wanachopaswa kufanya. Imetabiriwa wangepanya hivyo, kwa hiyo wa—watalifanya. Hakuna njia ya kuepa jambo hilo. Wakati wa Laodikia utafanya jambo hilo hilo.

¹⁰² Sasa mwangalieni. Huyu hapo amesimama pale, naye akasema, “Sasa, hatujakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne, na huyu hapa Mtu anayeniambia kwamba mimi ni nani, na kwamba baba yangu mcha Mungu alikuwa ni nani. Huyu ni Masihi.” Sasa, tunaambiwa ya kwamba Simoni alikuwa ni mtu asiye na elimu wala maarifa, bali alifanywa kiongozi wa Kanisa.

¹⁰³ Tunaona, palikuwa na mmoja aliyekuwa amesimama pale, jina la—lake ni Filipo, naye aliona jambo hilo. Naye alikuwa amefanya masomo ya Biblia pamoja na mtu a—aliyeitwa Nathanaeli. Kama ukiangalia mahali Yesu alipokuwa, hadi pale alipomwona Nathanaeli, ilikuwa ni maili kumi na tano. Hiyo ni safari ya siku nzima. Kwa hiyo hapana budi alikimbia kwenda kule, akazunguka kilima, namna hiyo. Sasa tutaona. Yeye alisema, “Nathanaeli!” Wakati alipokutana naye, alisema, “Unajua, tumekuwa na masomo ya Biblia.”

“Ndiyo.”

¹⁰⁴ “Vema, sasa, tumekuwa tukiamini ya kwamba wakati umewadia kwa jambo fulani kutukia. Vipindi vya nyakati vinabadilika, na tuko wakati wa Kuja kwa Masihi, maana hatujakuwa na nabii yeyote sasa kwa muda wa miaka mia nne. Na Malaki alitwambia ya kwamba Yeye angemtuma mtangulizi mbele yetu, nami ninaamini kwamba huyo ni Yohana.”

¹⁰⁵ Sasa tunajua, wakati unapoona ishara, ishara ya kweli ya Biblia, kuna sauti ya kweli ya Biblia nyuma yake. Kama hakuna sauti inayoifuata ishara hiyo, ni sauti ile ile tu ya kale ya kitheolojia, isahau; haikutoka kwa Mungu kamwe. Ipo, siku zote. Alimwambia Musa, “Kama hawataamini ishara ya kwanza, wataamini sauti ya ishara ya pili.” Hapana budi kuwepo na sauti pamoja na ishara. Kweli kabisa! Na kama ni sauti ile ile ya kale ya kitheolojia, isahau. Tayari mmekuwa na hiyo. Ni kitu fulani; Mungu anajaribu kuuvutia usikivu wa watu, kwa ishara, halafu anawapa sauti, kile kilicho nyuma ya ishara hiyo. Haina

budi kuwa ni sauti ya Kimaandiko; Musa asingeweza kuiamini, wala Paulo.

¹⁰⁶ Akiwa njiani mwake kwenda Dameski, wakati alipoiona ile ishara, ya ile Nguzo ya Moto, yeye alipaza sauti kwa nguvu, “Bwana!” Myahudi huyu kamwe asingeweza kuita kitu kingine chochote “Bwana,” ila Bwana, ila Bwana Mwenyewe. Yeye alisema, “U nani Wewe?”

¹⁰⁷ Yeye alisema, “Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kuipiga mateke michokoo.” Unaona? Kulikuwa na ishara, na kulikuwa na sauti ya ishara.

¹⁰⁸ Halafu angalia yale aliyosema. Angalieni, angalieni huduma yake tangu wakati huo na kuendelea, yale aliyofanya, nanyi mtaona jinsi ya kuliendesha kanisa.

Sasa tunaona, ya kwamba, hapo Yeye alitambulishwa kwa Simoni.

¹⁰⁹ Ndipo tunamwona, Nathanaeli, tutamleta huku. Naye Nathanaeli alisema, “Sasa, ngoja kidogo. Sasa, hapana shaka umekosea.”

¹¹⁰ “La, sijakosea. Je! unamjua yule mzee mvua samaki tuliye kuwa tukivua pamoja naye kule chini?”

“Naam.”

“Unajua yeye hakuweza kuandika jina lake.”

“Hiyo ni kweli, kwenye ile risiti, kwa ajili ya samaki wakati ule.”

¹¹¹ “Wakati alipokwenda Mbele ya Huyu ninayemjua kwamba ni Masihi. . . Sasa, ninataka kukuuliza, Nathanaeli. Wewe ni msomi mzuri, Mwebrania mzuri, na msomaji mzuri wa Biblia. Masihi atakuwa nini wakati atakapokuja?”

“Vema, Yeye atakuwa ni nabii, maana Biblia ilisema Yeye. . .”

¹¹² “Vema, ungesema nini kama nikikwambia ya kwamba alimwambia mtu yule, Simoni, kwamba alikuwa ni nani, na kwamba nanii yake, kwamba baba yake alikuwa ni nani?”

“Loo, siwezi kuamini hilo.”

“Vema, hebu na twende tukaone. Hebu twende. Njoo uone.” Unaona?

“Je! kitu chochote chema kinaweza kutoka Nazareti?” akasema.

¹¹³ Akasema, “Njoo uone.” Hilo ni swali jema. Usikae nyumbani na kulikosoa. Njoo ujionee, mwenyewe. Akasema, “Njoo, lete Biblia yako na uichunguze.” Huyu hapa anakuja.

“Laweza neno jema kutoka Nazareti?”

Kasema, “Njoo, uone.”

114 Na wakati alipoenda Mbele za Yesu, Yesu alimwangalia. Sasa Yeye akasema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Rabi, ulipataje kunitambua?”

115 Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.”

116 Akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Ndiwe Mfalme wa Israeli.”

117 Kwa nini? Tabia Yake ilimtambulisha. Kwa nini? Waebrania mlango wa 4, kifungu cha 12, inasema hivyo, “Neno la Mungu lina nguvu zaidi, lina ukali zaidi kuliko upanga ukatao kuwili, linagawanya, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.”

118 Hivyo ndivyo manabii walivyofanya, nao walikuwa Neno. Walikuwa ni Neno katika wakati wao, lakini hapa alikuwapo utimilifu wa Neno. Unaona? Hao ndio wangewaambia ni kitu gani kilitukia, kuyatambua mawazo; na yaliyokuwapo, yaliyopo, na yatakayokuja.

119 Kwa hiyo huyo hapo amesimama pale. Loo, kulikuwa na baadhi yao waliosimama pale, wakasema... Iliwabidi kutoa jibu kwa kusanyiko lao. Iliwabidi kufanya hivyo, maana pale ka—kazi kuu zilikuwa zimefanywa wala wasingeweza kukana jambo hilo.

120 Unaona, tayari walikuwa na uponyaji, kuhusu uponyaji. Walikuwa na Birika la Bethsaida, huko juu, mnajua. Wao, Bethsaida, waliingia kwenye birika hilo na wakaponywa. Walikuwa na uponyaji wa Kiungu katika kila wakati, bali hapa alikuwapo nabii.

121 I—iliwabidi kufanya jambo hilo. Unajua walivyosema? “Mtu huyu ni Beelizebuli, mpiga ramli. Anafanya ninii. . .”

122 Yesu alisema, “Nitawasamehe kwa jambo hilo. Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja katika wakati mwingine, kufanya Neno lilo hilo, kazi moja... neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe, si katika ulimwengu huu au ulimwengu ule ujao.” Huko ni kukufuru, kumwita Roho wa Mungu pepo mchafu, ambaye anafanya kazi ya Mungu. Wazia jambo hilo kwa makini sana sasa. Kumbukeni, weka hilo niani mwako.

123 Naam, hivyo ndivyo alivyotambulishwa jana. Huyo alikuwa ni Yesu, jana. Na kama Yeye ni yeye yule leo, Yeye angefanya jambo lile lile. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha kama Masihi. Hivyo ndivyo walivyomjua, kwa kazi hiyo. Angalia, hiyo ni. . .

124 Kuna aina tatu tu, jamii tatu za watu, hizo ni, Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Na hao ni—ni watu wa Hamu, Shemu na Jafethi. Sasa, kama tunaamini Biblia, wote wanatokana na wana wa Nuhu, na huyo ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

¹²⁵ Sasa, Mmataifa hakuwa akitazamia Msama-...Masihi yeyote. Tulikuwa na rungu mgongoni mwetu, na tukiabudu mungu wa kikafiri. Sisi Waanglo-Saxon, na kadhalika, katika siku hizo, tulikuwa makafiri, Warumi na Wayunani, na kadhalika. Hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote. Lakini Waebrania walikuwa wakimtazamia, Naye...

¹²⁶ Kumbukeni, shikeni hili vizuri sasa. Yeye anawatokea tu wale wanaomtazamia. Yeye huwatokea tu wale wanaomtazamia. Anajitambulisha kwa wale wanaomtazamia.

¹²⁷ Naye alijitambulisha kwa Wayahudi, mara nyingi. Wakati tutakapofikia baadaye juma hili, tuwachukue watu wengine zaidi. Lakini sasa hivi...

¹²⁸ Sasa kuna Msamaria, wao wanamtazamia, pia. Kwa hiyo Yeye alikuwa akienda zake Yeriko, kwa hiyo ilimbidi apitie Samaria, ndipo akaja kwenye mji wa Sikari. Yapata saa tano, ama saa sita, Naye akawatuma wanafunzi mjini, wakanunue vyakula.

¹²⁹ Walipokuwa wameondoka, mwanamke mwenye sifa mbaya wa mji huo alijitokeza, labda ni msichana mrembo. Yeye alikuwa labda, mwajua, alikuwa amefukuzwa na wazazi wake na kila kitu, naye hakuwa ameona kitu chochote kanisani, kwa hiyo alipata tu riziki yake kwa njia mbaya, kwa kuwa na wanaume wengi mno. Naye akaja kisimani, na hapo alikuwapo Yesu ameketi pale, Myahudi.

¹³⁰ Labda alionekana ni mzee kidogo kuliko vile alivyokuwa kweli, maana Yeye alikuwa na umri wa miaka thelathini tu, nasi tunaona katika Yohana Mtakatifu 6 ya kwamba walidai ya kwamba alionekana kana kwamba alikuwa na umri wa miaka hamsini. Wao walisema, "Wewe hujapata bado miaka zaidi ya hamsini, na unasema umemwona Ibrahimu?"

¹³¹ Akasema, "Yeye Ibrahimu asijakuwako, Mimi Niko." Mnaona? Lakini huenda ilikuwa, kazi Yake, huenda ilimchosha sana.

¹³² Huyu hapo alikuwa, ameketi akiegemea ukuta, ndipo mwanamke huyu akaja na kuchukua ninii ndogo...Ninyi mlio na, huku Kusini, silingi, mwajua, na kuzingirisha. Kungali kuna visima vidogo kule vya kale, na vingali viko vile vile. Na ni mandhari ndogo, inavyoonekana. Na—naye akashusha ndoo hii ya maji.

¹³³ Unapaswa kuwaona hao wanawake. Ninyi wanawake mnazungumza juu ya kutembea vizuri! Nimewaona wamebeba mitungi hiyo, ambayo inabeba kama galoni tano, nao wanaichukua na kuiweka juu ya kichwa chao, mmoja huko juu. Wanaweka mmoja kwenye nyonga moja, na mwingine kwenye hiyo nyingine, na wanatembea moja kwa moja, wakizungumza, bila kumwaga hata tone. Wanatembea tu vizuri tu ulivyowahi kuona.

134 Sasa huko Mashariki, unaona, wanawake wabaya na wanawake wazuri hawawezi kushirikiana. Ni tofauti hapa, bali—bali hawawezi kule. Yeye ametiwa alama, ametiwa alama. Hivyo tu. Kama akipata kuwa na mume asiyefaa, hawachangamani naye tena. Lakini kule...Yote yamechanganywa pamoja hapa sasa, tunaona, lakini kule hayakuwa yamechaganywa.

135 Kwa hiyo yeye asingeweza kuambatana na mabikira, wa asubuhi. Ilimbidi kuja yapata adhuhuri, kuteka yake, maji.

136 Kwa hiyo akaanza kushusha mtungi wake wa maji. Lakini hapo palikuwa na mbegu iliyokusudiwa tangu zamani ndani ya maskini mwanamke huyo. Alishusha mtungi huo wa maji, ndipo akamsikia Mwanamume mmoja akisema, “Nipe maji ninywe. Nilettee maji ninywe.”

137 Huyu mwanamke akageuka akaangalia kote, akamwona Myahudi huyu. Naye Myahudi huyu, labda, ni Mtu mwenye umri wa makamu. Sijui ni nini kilichokuwa mawazoni mwake wakati huo. Kwa hiyo akasema, “Mbona, si kawaida Kwako, ukiwa Myahudi, na uniombe, mwanamke wa Samaria.” Unaona, hakujua ilikuwa ni—ilikuwa ni nini. Yeye alininii tu...labda mtu huyo labda anamchezea, kwa hiyo yeye...Kasema, “Si kawaida kwenu ninyi Wayahudi.”

138 Na kwa hiyo mazungumzo yakaendelea. Yeye alikuwa akijaribu kufanya nini? Alikuwa akijaribu kuvutia usikivu wake. Baba alikuwa amemtuma sehemu zile, lakini sasa ilimbidi kutaka kujua ni kwa nini kule.

139 Walikuwa wakimtarajia Masihi. Alikuwa tayari amejitambulisha na Wayahudi, sasa ndiye huyu hapa pamoja na—pamoja na—pamoja na Wasamaria.

140 Naye akasema, “Si kawaida kwako ku—ku—kuniomba mimi, mwanamke wa Samaria, kitu kama hicho.”

141 Kwa hiyo akasema, “Lakini kama ungelijua ni Nani uliyekuwa ukiongea Naye, ungeniomba maji unywe. Nitakupa maji usije hapa kuchota.”

142 Ndipo wakaendelea kuongea juu ya ibada. Papo hapo akapata shida yake ilikuwa ni nini. Sote tunajua ilikuwa ni nini, wanaume wengi kupita kiasi. Akamwangelia, akasema, “Mwanamke, nenda ukamwite mume wako mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

143 Akasema, “Umesema kweli, kwa maana umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

144 Mwangalie mwanamke huyo. Angalia tofauti kati yake na dhehebu hilo. Mwangalie kama mtu binafsi. Waangalie hao Mafarisayo, walisema, “Mtu huyu ni Beelizebuli.” Mwangalie. Si yeye.

¹⁴⁵ Aligeuka, naye akasema, “Bwana, ninaona kwamba Wewe u nabii.” A-ha, hiyo hapo ile Nuru, unaona. Wakati Mwana atakapoigusa hiyo Mbegu, na ni ya aina nzuri, italeta Uzima, kwa hakika tu kama kuwapo kwa dunia. Aliigusa ile Mbegu katika moyo wa maskini kahaba huyo! Akasema, “Bwana, ninaona ya kwamba Wewe u nabii. Sasa tunajua ni ninii... Tumekuwa na mamia ya miaka tangu tulipokuwa na nabii. Nasi tunajua ya kwamba atakapokuja Masihi. Tunamtazamia. Na atakapokuja Masihi, jambo hili ndilo atakalofanya.”

¹⁴⁶ Hiyo ndiyo ishara ya Masihi. Je! hamwoni? Ilikuwa ni Masihi aliyekuwa katika Musa. Ilikuwa ni Masihi aliyekuwa katika Henoko. Ilikuwa ni Masihi katika kila wakati. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni Kristo wakati wote.

¹⁴⁷ Kasema, “Ninajua. Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, hivyo ndivyo atakavyofanya.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Loo, jamani!

¹⁴⁸ Kwa hilo, aliangusha mtungi wa maji, akakimbilia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia yale niliyofanya. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹⁴⁹ Na watu wa mji huo, bila ya kuona likitendwa, mji mzima ulimwamini. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Tabia ya vile alivyokuwa. Yeye alitambulishwa kwa mji ule wa Sikari. Alitambulishwa, Masihi wa Mungu, kwa tabia Yake, tabia iliyokuwa ndani Yake. Maana, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni Mungu wa manabii. Alikuwa ndiye Nabii yule. Alikuwa ni Nabii aliyeidhihirishwa. Daima amekuwa, kote katika wakati, yeye yule, na kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Sasa kuharakisha na kufunga.

¹⁵⁰ Tunaambiwa, katika Zekaria 14:6 na 7, ya kwamba, “Kutakuwako na siku,” nabii alitabiri, “ambazo haziwezi kuitwa usiku wala mchana. Ni siku yenye utusitusi, huzuni, giza, “lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.” Biblia ilisema hivyo.

Sasa angalia, katika kufunga.

¹⁵¹ Kijiografia, jua huchomoza kwa watu wa Mashariki, kwanza. Linachomoza Mashariki na kutua Magharibi. Sasa nifuatilieni kwa makini. Ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Sote tunajua jambo hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁵² Vivyo hivyo na Injili. Injili ilianza Mashariki. Ilitokea Mashariki; ikavuka, ikaingia Ujerumani, ikavuka Mediterranean, ikaingia Ujerumani; kutoka Ujerumani, ikavuka Mlangobahari wa Uingereza, ikaingia Uingereza; kutoka huko, ikavuka Atlantiki, ikaingia Marekani, kwenye Pwani ya Mashariki; na imesafiri hadi kwenye Pwani ya Magharibi. Sasa Mashariki na Magharibi zimekutana.

153 Na jua lile lile linalochomoza Mashariki, ni jua lile lile linalotua Magharibi.

154 Sasa angalia. Mwana, M-w-a-n-a, alichomoza kama Masihi, kwa watu wa Mashariki.

155 Na sasa tumekuwa na siku, tangu kuondoka Kwake, ya madhehebu na kukutana pamoja, na—na kadhalika. Tumekuwa na nuru ya kutosha kama siku yenye utusitusi wakati jua limefichwa na mawingu. Nao wamekuwa na madhehebu. Tumejenga hospitali. Tumejenga shule. Tumejenga madhehebu. Tumefanya mambo haya yote jinsi hasa tunavyopaswa kufanya.

156 Lakini Yeye alisema, “Wakati wa jioni itakuwa Nuru.” Yesu yeye yule, katika nguvu Zake za kufufuka, atafufuka tena, kama alivyoahidi katika Malaki 4, kama alivyoahidi katika Yohana Mtakatifu 14:12. Kama alivyoahidi katika Luka 17. “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

157 Angalia kilichotukia katika siku za Sodoma. Ibrahimu, yule aliyekuwa na ahadi ya mwana atakayekuja, hapa tunamwona kule, nasi tunaona ishara iliyofanywa.

158 Kule chini Sodoma, tuliona kile kilichotukia. Na unajua kamwe hatujaninii. . . Sasa, kule, Lutu alikuwa ni mfano wa kanisa la kawaida, kule chini Sodoma, dhehebu, nao walimpata mjumbe chini kule. Kulikuwako na baadhi ya wajumbe walioenda huko chini, Billy Graham na Oral Roberts wa kisasa. Na je! mnajua nini? Hakuwapata kuwa na wakati, katika historia ya kanisa, ambapo mtu alipata kutumwa ulimwenguni kote kwa kanisa, ambaye jina lake linaishia na h-a-m, mpaka wakati huu. Billy G-r-a-h-a-m, herufi sita. A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba. Lakini Billy G-r-a-h-a-m yuko moja kwa moja huko Sodoma, akibishabisha kwa nguvu na kuwaita.

159 Lakini, kumbukeni, kulikuwa na mmoja kwa kanisa la kiroho, aliyekuwa nje, Ibrahimu aliyeitwa atoke. Angalia alitoa ishara ya namna gani. Hakuhubiri Injili nyingi; aliwaambia tu ni ahadi gani zilikuwa ziwe. . . Naye akasema, “Yuko wapi Sara?” Sasa, kumbukeni, alikuwa Sarai siku moja hapo kabla, naye alikuwa Abram siku moja hapo kabla. Sasa Yeye alisema, “Ibrahimu, A-b-r-a-h-a-m, yu wapi S-a-r-a?” sio S-a-r-a-i. “Yu wapi Sara, “binti mfalme,” mkeo, baba wa mataifa?”

Akasema, “Yuko kwenye hema, nyuma Yako.”

160 Pia akasema, “Nitakurudia wakati huu huu mwakani.”

161 Mtu aliyekula nyama ya ndama, akanywa maziwa toka kwa ng’ombe, na akala ugali, akinywa maziwa. Mtu, mavumbi nguoni Mwake, naye ameketi pale ameelekeza mgongo Wake hemani. Kasema, “Yuko wapi mkeo Sara?”

Kasema, “Yuko kwenye hema, nyuma Yako.”

¹⁶² Naye Sara akasema, “Mimi, mwanamke mzee kama nilivyo, mwenye umri wa miaka mia moja, kama mume na mke walikuwa wamekoma muda mrefu. . . kuwa na raha na bwana wangu, naye ni mzee, pia?” Biblia ilisema “wazee sana,” imekuwa miaka na miaka. Alikuwa na miaka arobaini na mitano baada ya kukata hedhi, ama zaidi ya hiyo, labda miaka hamsini na mitano baada ya kukata hedhi. “Nami niwe na raha na mume wangu, kama msichana?” Alicheka moyoni mwake, mwajua.

¹⁶³ Na, hilo, Mwanamume huyo, Mtu huyo katika mwili wa kibinadamu, kasema, “Kwa nini Sara amecheka?”

¹⁶⁴ Ni kitu gani kilichotukia? Ibrahimu alimwita Mtu huyo, “Elohimu,” Mwenyezi Mungu akiwakilishwa katika mwanadamu.

¹⁶⁵ Yesu Bwana wetu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kule Kuja,” na angalieni, “wakati Mwana wa Adamu anafunuliwa, kutambulishwa,” Luka 17. “Wakati Mwana wa Adamu, katika siku za mwisho, anafunuliwa. Mwana wa Adamu akifunuliwa, Injili Yake inamtambulisha kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.”

¹⁶⁶ Angalia vile wanavyofanya sasa, mataifa yaliyopotoshwa. Loo, jamani! Waangalie walawiti, na angalieni yale tuliyo nayo sasa. Kanisa ni katika mchafuko. Taifa liko katika mchafuko, na kitu hicho chote. Mungu anakitapika, kutoka juu, chini ya ardhi. Kitu hicho chote ni mchafuko.

¹⁶⁷ Kijiografia, na pia kimaumbile, jukwaa limeandaliwa. Si ni wakati wa Mungu kurudi katika mwili wa kibinadamu, “Neno lililo kali kuliko upanga ukatao kuwili, na linalotambua mawazo na makusudi ya moyo,” kujitokeza jukwaani, kumfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! Ni Neno lililoahidiwa lililogawiwa kwa siku hii. Tunaishi katika siku hii, na Mungu yupo hapa pamoja na sisi, kulidhihirisha hilo na kulifanya kweli.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁶⁸ Baba wa Mbinguni, Wewe ulisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Tunakuona Wewe, Bwana, kwa ishara zote; mataifa yanavunjika; Israeli wako kwenye nchi ya uenyeji wao; matetemeko ya nchi mahalimahali; mioyo ya watu ikivunjika; akili zilizopotoshwa; wamekataliwa kwa mambo ya Kweli. “Kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa,” Wewe ulisema, “watu walioharibika akili zao, waliopewa nguvu za upotevu, ili wauamini uongo na wahukumiwe kwa huo.” Lakini Wewe uliahidi, katika siku hiyo, ya kwamba utajitambulisha, Mwana wa Adamu angefundiwa, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa tabia Yake ile ile iliyomtambulisha katika kila wakati.

¹⁶⁹ Jalia Yeye, usiku wa leo, Bwana Mungu, Yehova mkuu, Elohimu, ushuke ndani ya watu Wako, usiku wa leo, Bwana.

Shuka na ujitambulishe Mwenyewe, kusudi waaminio wapate kuamini. Kusudi watu wafahamu na kujua ya kwamba Wewe ungali unabaki kuwa Mungu, nawe ni Wewe yeye yule jana, leo, na hata milele. Halafu basi, Bwana, wale waliokusudiwa uponyaji, na hao waliokusudiwa Uzima wa Milele, watanyosha mkono na kushika, Bwana, kwa kuwa huu ni wakati wa kuzuriwa. Jalia usipite bure. Ninaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

170 Ni wangapi wanaoamini ya kwamba hiyo ni kweli, hiyo ni Injili? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa je! tunaishi katika siku hiyo? Hilo ndilo jambo linalofuata. Kama ndivyo ilivyo, Mungu anawajibika kwa uchaji kulitambulisha.

171 Sasa endapo mtanipa usikivu wenu mkamilifu. Nitachelewa tu kidogo, niliwaambia usiku wa leo, labda dakika kumi na tano.

172 Tuliwapa kadi za maombi. . . Za A, za A. Vema, hebu tuanze upesi sana. A, namba moja. Nitawaita tu mmoja kwa wakati mmoja, mpate kusimama papa hapa, mkiweza. A, namba moja. Ni nani aliye na kadi ya maombi A, namba moja, inua mkono wako? Sasa kama huwezi kusimama, nitaninii. . . baadhi yao watakuja kukuchukua. A, namba moja, vema. Sasa njoo mara unapoitwa, namba yako tu. Vema, A, namba moja. Vema.

173 Namba mbili, ungeweza kuinua mkono wako? Namba mbili, kadi ya maombi A, namba mbili, inua mkono wako. Waweza kuja, mama? Sasa kama kuna mtu aliyelemaa wala hawezi kuamka, mabawabu watakubeba. Namba mbili.

174 Tatu, inua tu mkono wako. Itaokoa wakati, upesi sana, kama utaita. . . Namba tatu, waweza kuinua mkono wako? Papa hapa, mama. Namba nne, inua mkono wako, namba nne. Maombi. . . Namba nne, njoo. Vema. Namba tano, kadi ya maombi namba tano. Papa hapa, mama. Namba sita.

175 Aha? Hivi anaweza kutembea? Sawa. Hiyo ni. . . Ama, mpelekee kiti kule chini. Mama huyo ni mgonjwa, nafikiri, ama labda mumewe, ama yeyote yule aliyekuwa ameketi pale pamoja naye. Ama ni ninii. . . Mpelekeeni kiti pale, yeye. . . Vema.

176 Namba saba, Namba nane. Namba tisa, tisa. Ninapata. . . Naam, hapa, tisa, tisa. Kumi, namba kumi, kadi ya maombi namba kumi? Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na tatu, kumi na nne. Shuka uende kwenye ule mwisho mwingine kule chini, ile ya kumi na nne. Kumi na tano. Vema, nenda—nenda moja kwa moja nyuma yao.

177 Sasa ngoja tu kidogo mpaka hawa waingie mstarini, tuone mahali tulipo hapa kwa muda kidogo tu. Sasa ninyi wengine shikilieni kadi zenu kwa muda kidogo tu.

178 Sasa ni wangapi kwenye kusanyiko hili ambao ni—ni wagonjwa, na hawana kadi ya maombi? Inueni mikono yenu namna *hii*. Vema. Kila. . . Sijali mko wapi. Vema.

¹⁷⁹ Sasa iweni tu na uchaji. Sasa, angalieni, wakati wakipanga mstari wa maombi, ninyi nyote nisikilizeni kwa makini sana sasa. Inawabidi kusikiliza yale ninayowaambia. Mnaona? Angalieni.

¹⁸⁰ Wakati mmoja kulikuwako na mwanamke, Yesu alikuwa akipitia nchini naye akavuka bahari, kisha akaingia mahali fulani na kulikuwa na mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu. Na makuhani wote na hao wengine walikuwa wametoka nje, walikuwa wakimdhahi, bila shaka. Na kulikuwako na kundi moja kule nje waliomwamini. Naye alikuwa akipita katikati ya umati. Ndipo yule mwanamke akasema moyoni mwake. . .

¹⁸¹ Sasa sikilizeni kwa makini sasa. Je! mnasikiliza? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Hii, sasa, mwanamke huyo. . . Mnaona, juu ya chochote, unakatiwa yale unayofanya, unaona. Kila mtu ni ninii. . . Sikushughulikii kama mwi—mwili. Ninakushughulikii kama roho, nafsi. Unaona? Na kusonga huko, akili yako inaelekea mahali pengine, unaona, ninajaribu kuishika hiyo. Angalia sasa, kulikuwa na mtu aliyemwalia Paulo, akiamini kwa dhati; Paulo akasema, “Ninaona una imani ya kuponywa.” Unaona? Sasa angalia.

¹⁸² Mwanamke huyu, alipokuwa akipitia hapa, asingeweza kumfikia. Kila mtu alikuwa akimkumbatia, kila kitu. Hebu tuseme, kwa kusema tu—kwa kusema tu sasa, yeye hakuwa na kadi ya maombi wala asingeweza kuingia mstarini.

¹⁸³ Na kwa hiyo, kila mtu, “Aloo, Rabi! Wakisema, je! Wewe ndiwe yule nabii? Tu—tunaamini ya kwamba yuja nabii, bali mimi—mimi sikujui. Unaona, si—sina hakika. Nitafukuzwa kanisani mwangu kama ningeamini Hilo.” Unaona? Na, unajua, ni hadithi ile ile tu ya kale ikijirudia.

¹⁸⁴ Kwa hiyo basi maskini mwanamke huyu, yeye aliamini jambo hilo. Kwa hiyo alijipenyeza, na akasema, “Kama ninaweza kugusa upindo wa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Kwa hiyo akamgusa.

¹⁸⁵ Sasa kama mtu yeyote alipata kuona vazi la Kipalestina, una vazi la ndani, halafu vazi la nje linapwaya. Sasa, kama mwanamke fulani aligusa koti la mmoja wenu wanamume, upindo tu wa koti lako, namna *hiyo*, kisha akaondoka akaenda zake, usingeweza kamwe kujua hilo katika kundi kama hilo. Vipi kuhusu vazi hilo kubwa linalompwaya *hiyo* bila kumgusa? Naye alikuwa amepiga magoti na kugusa tu vazi Lake, kisha akarudi nyuma.

Yesu alisimama. Akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

¹⁸⁶ Basi angalia vile Petro alivyosema, sasa, akiwa na funguo za Ufalme. Kwa maneno mengine, hebu na tuliweke kwa maneno yetu ya siku hizi, “Mbona, Bwana, unasema baadhi ya mambo mabaya sana! Vema, hao watu watafikiri ya kwamba Wewe una kichaa, kuna kasoro fulani. Kila mtu amekugusa.”

¹⁸⁷ Kila mtu alisema, “Aloo, Rabi! Aisee, je! Wewe ndiwe mponyaji wa Kiungu? Ndivyo wanavyosema. Unasema . . . Ngoja, nina uwanja wa makaburi yaliyojaa watu hapa, kama unataka kumfufua mmoja kwa ajili yetu. Njoo huku, nasi tutakuamini kama utafanya jambo hilo.” Na wengine tu wakimuunga mkono na wengine wakimpinga, kama tu ilivyo katika kila kundi, unaona; na wakimdhihaki, na wengine wakimwamini.

¹⁸⁸ Naye Petro akasema, “Mbona, kila mtu anakugusa! Kwa nini useme jambo kama hilo?”

¹⁸⁹ Yeye akasema, “Lakini naona ya kwamba nimekuwa dhaifu; nguvu zimenitoka,” huo ni uweza.

¹⁹⁰ Angalia, Yeye alitazama kote kwa wasikilizaji na akampata maskini mwanamke huyo. Asingeweza kuficha hilo. Unaona? Yeye alikuwa na ile mbegu imekaa mle ndani. Ee Mungu, tupe hiyo Mbegu! Hiyo ndiyo tunayohitaji sasa hivi. Yeye alimpata, Naye akamwambia juu ya kutokwa kwake damu. Kasema, “Imani yake ilikuwa imemponya.”

¹⁹¹ Angalia, unasema, “Kwamba, kama Yeye angalikuwa hapa usiku wa leo, ningefanya jambo lile lile.” Kama angetembea kupitia kwenye jengo hili, usiku wa leo, je! unaamini kama ungemgusa ungeponywa?

¹⁹² Vema, hebu nikwambie. Katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 3, kinasema ya kwamba, “Yeye sasa hivi ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.” Ni wangapi wanaoamini hilo ni Kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaona? Vema, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye angetendaje leo? Kama vile alivyofanya jana. Hiyo ni kweli? [“Amina.”]

¹⁹³ Sasa si lazima kuwapo hapa juu. Amini tu, na useme hivi, “Sasa, Bwana, mi—mimi. . . Haya yote ni mageni, lakini mtu huyu anayasema kutoka katika Biblia. Yanasikika. . .” Yalisikika ya kigeni katika kila wakati. Lakini yatafutuni, muone kama Maandiko. . .

Yesu alisema, “Yachunguzeni Maandiko, Hayo yananishuhudia Mimi.” Mnaona?

¹⁹⁴ Sasa yachunguzeni Maandiko. Hiyo ni kweli. Tuko katika siku za mwisho. Maumbile yote yanathibitisha ni siku za mwisho. Kanisa liko katika machafuko yake, nyote mnaelekea kwenye yale mauaji makubwa mno ya ekumeni hivi karibuni sana, hapa juu, mnaona, mama kahaba tu na binti zake wote, kama tu—kama tu Biblia ilivyosema, kuchukua alama ya mnyama wala hamjui. Mnaona? Loo, tutafikia jambo hilo baadaye.

¹⁹⁵ Angalia sasa, wakati Yeye akiwapo, kama tunaweza kupata Uwepo Wake hapa. Ninyi mlio huko nje bila kadi ya maombi, guseni vazi Lake. Yeye ni Kuhani Mkuu. Mnafanyaje jambo

hilo? Kwa imani yenu? Guseni vazi Lake mwone kama Yeye hageuki na kufanya jambo lile lile alilofanya wakati huo. Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Hilo lingekuwa ni la kushawishi sana. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

¹⁹⁶ Sasa, kila mtu, mtu ye yote asisogee popote sasa. Iweni na kicho sana. Mnaona, hamna budi kumheshimu Roho Mtakatifu. Heshima! Njia pekee utakayopata chochote kutoka kwa Mungu, ni kuuheshimu Ujumbe Wake. Uheshimu. Sasa sikilizeni.

¹⁹⁷ Hebu na tuwachukue tu, ninyi nyote Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, na Katoliki, na wote, chukueni tu dini zenu, dhehebu lakho, na uliweke hapa kwa, kando, dakika chache, na kusema, “Kama Yeye ni Neno, Neno huyatambua mawazo yaliyo moyoni. Huyo alikuwa ni Masihi jana; huyo ni Yeye leo. Haina budi kuwa. Naye aliliahidi hilo leo, sasa.”

¹⁹⁸ Sasa huyu hapa maskini mama mmoja amesimama hapa. Sasa mtu ye yote asisogee. Iweni tu na uchaji na msimame kimya. Sasa mimi, kwa—kwa karama . . .

¹⁹⁹ Sasa, karama si kitu tu unachochukua kama shoka la kukata, na unaenda ukikatakata na kupasua. Hilo ni kosa. Karama ni kujua jinsi ya kujiondoa njiani. Ni kujipumzisha mwenyewe tu na kujiondoa, ndipo basi Mungu anaingia na kukutumia jinsi anavyotaka. Karama ni kujiondoa njiani. Unaona? Si kitu fulani unachotia mkononi mwako, unaenda ukikata na kuchoma; huyo, huyo si Mungu. Mnaona? Jambo tunalofanya ni kujiondoa tu njiani, ndipo Roho Mtakatifu anaingia na kuanza kuitumia jinsi anavyotaka kuitumia.

²⁰⁰ Sasa inakubidi kujiondoa njiani. Haidhuru Mungu angefanya nini hapa, Yeye hana budi kukufanyia hilo, pia. Haidhuru angenitia mafuta kiasi gani, Yeye hana budi kukutia mafuta wewe. Kama hakutii mafuta, “hakuweza kufanya miujiza mingi.”

²⁰¹ Sasa ninaamini nimemwona mtu mmoja, mvulana mdogo, jinsi ilivyoonekana, ameketi hapa kwenye kiti cha magurudumu ama kitu fulani. Nikafikiri nilimwona mtu kule nyuma. Haidhuru ni kitu gani, mahali ulipo, sasa wewe amini tu. Huyu hapa maskini mwanamke mmoja ameketi hapa, ameinamisha kichwa.

²⁰² Sasa kumbuka, siwezi kumponya mtu yeyote. Hakuna kitu kama mtu yeyote kuponya. Ni Mungu. Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo sasa? [Kusanyiko linasema “Amina.”—Mh.] Uponyaji umenunuliwa tayari. Ni kuwafanya mwamini ya kwamba Uwepo Wake upo hapa kutimiza Neno Lake. Sasa kama nimewaambia Neno Lake, ya kwamba Yeye aliahidi kufanya jambo hili, nanyi nyote mnaamini jambo hilo; sasa kama Yeye akifanya jambo hilo, hilo linamtambulisha hapa.

203 Sasa huyu hapa mwanamke amesimama hapa, mama kijana. Yeye ni mdogo kuliko mimi. Na hii hapa picha ya Yohana Mtakatifu 4, mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara ya kwanza. Sisi hatufahamiani, nadhani, ewe msichana, (sivyo?) sisi kwa sisi. [Huyo dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Hatufahamiani. Sasa ninataka wasikilizaji waangalie. Mimi simjui. Sijapata kumwona. Mlimsikia akisema tu jambo hilo hivi punde. Simjui. Yeye hanijui. Sisi hapa tumesimama.

204 Sasa huenda akawa ni mgonjwa. Huenda ikawa ana shida ya pesa. Huenda ikawa ni matatizo ya kinyumbani. Huenda ikawa ni kwa ajili ya mtu mwingine. Sina fu—fununu yoyote hata kidogo. Simfahamu mwanamke huyu, sijapata kumwona.

205 Lakini kama Kristo angekuwa amesimama hapa, akiwa amevaa suti hii, ambayo Yeye alinipa, sasa... Na kama tuseme yeye ni mgonjwa, kama yeye angesema, “Bwana, je! utaniponya?” Mbona, Yeye angejibu moja kwa moja, pia, Yeye hawezi kufanya la zaidi, na kumwambia Yeye amekwisha mponya. [Dada huyo anasema, “Mungu asifiwe!”—Mh.] Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Mnaona? Asingeweza kumponya...

206 Lakini Yeye angeweza kujitambulisha Mwenyewe kama Masihi. Angejua jambo hilo, kwa maana Yeye angefanya hivyo, angekuwa na tabia ile ile. Sasa isingekuwa ni mimi kama Yeye alifanya hivyo, kwa maana...

207 Kwanza, ilikuwa ni Mungu katika Nguzo ya Moto, Mungu juu yetu; halafu Mungu pamoja nasi, katika Kristo; sasa Mungu ndani yetu, mnaona, wana wa Mungu, katika kule kufanywa wana ambako Kristo alikuja kufanya, kukomboa sifa za Mungu kama alivyofanya hapo mwanzo.

208 Sasa kama Neno Lake linakaa *humu* ndani, nami nimewaambia Kweli, na ndivyo ilivyo, nalo Neno limo humu ndani, moyoni mwangu, basi Mungu atajitambulisha Mwenyewe kwamba hilo ni Kweli. Basi hilo linapaswa kufanya nini kwa kusanyiko hili? Linapaswa kufanya nini, mnapoona Maandiko papa hapa mbele zenu? [Kusanyiko linashangilia.—Mh.]

209 Sasa, sasa sina budi kuzungumza na mwanamke huyu, maana nimekuwa nikihubiri. Kuzungumza naye kwa dakika moja tu, mpaka Roho Mtakatifu atakapoanza kutenda kazi, ndipo ninyi nyote anzeni kuamini. Sasa, nasi tutawaona kesho usiku, sasa. Unaona, hili hapa, uko—uko katika ulimwengu mwingine, kiwango kingine, unaninii tu... hujui kile kinachotendeka. Wewe, yeyote yule aliye kwenye maikrofoni, idumishe na sauti kubwa.

210 Sasa ninataka kuzungumza nawe tu kama Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke pale kisimani. Sasa, mimi ni mwanamume, nawe ni mwanamke, ni mara yetu ya kwanza kukutana duniani. Na—na sasa kama... Yeye

alimwambia, “Nataka unipe maji ninywe,” ama kitu kama hicho. Unakumbuka hadithi hiyo? Je! ulipata kuisoma hiyo katika Biblia? Umeisoma? Vema.

²¹¹ Sasa kama Bwana Yesu atafanya jambo lilo hilo usiku wa leo, kwa namna fulani atanifunulia shida yako ni nini, ama yale umefanya, ama—ama kilichokuleta hapa, ama kitu kingine kama hicho, ungejua ilibidi li—litoke kwenye nguvu fulani za kimbinguni. Je! ungeamini kwamba ni kile nimewaonyesha ya kwamba Maandiko yanasema kitakuwa? Tunaona matetemeko ya nchi, tunaona ulimwengu ukiwa katika machafuko haya, tunaona madhehebu jinsi yalivyo, na wakati umewadia kwa jambo hilo kutukia. Sivyo? Unaamini jambo hilo? Vema, sasa, kama Yeye angejitambulisha Mwenyewe kwa jambo hilo, huyo angepaswa kuwa ni Mungu. Isingewezekana kuwa ni mimi kama mwanadamu. Mimi ni ndugu yako tu.

²¹² Sasa, wewe ni Mkristo. Si kwa sababu unasema, “Bwana asifiwe.” Ungeweza kuwa ni mdanganyifu anayesimama pale, akisema hivyo. Unaona? Lakini, kama ndivyo ilivyokuwa, Yeye ange—ange—angejua jambo hilo. Unaona? Lakini ninasikia roho yako ikitetema. Ni kweli. Wewe ni Mkristo.

²¹³ Sasa, kama Bwana Yesu atanifunulia shida ya mwanamke huyu ni nini, ni wangepi wataamini sasa kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²¹⁴ Sasa niangalie, dada, dakika moja. Hili hapa linakuja. Unaona, sasa mimi ninanii tu. . . Inabidi iwe ni ono, unaona. Litabidi lilione kwa njia fulani, maana. . . Naam, bwana. Sasa Huyu hapa. Mungu asifiwe! Ninachukua kila roho, chini hapa sasa, chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Iweni na kicho. Angalia hapa kwa dakika moja, mama. Niangalie mimi. Sasa ni wakati wa Bwana kusema jambo fulani ama kufanya jambo fulani.

²¹⁵ Kama unahisi, kama umewahi kuona ile picha ya ile Nuru, imesimama kati yangu na mwanamke huyu. Naye yupo hapa, anaogua ugonjwa wa damu. Ni ugonjwa wa kisukari. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mnaona? Sasa vipi kama. . .

Huenda mtu fulani akasema, “Ulikisia hilo tu.”

²¹⁶ Angalia hapa, ewe msichana. Wewe ni mtu mzuri sana sasa. Angalia hapa. Je! unaamini mimi ni mtumishi wa Mungu? [Huyo dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Unaamini. Mimi siwezi kuponya. Wala sijui uliyoambiwa. Lolote lile, lilikuwa ni kweli, sivyo? Hili hapa jambo lingine. Ninaona m—msichana. Ni msichana mdogo ambaye unamwombea, ambaye ana kitu fulani sikioni mwake. Ni sikio linalovuja, hiyo ni kweli? Naam, naam, hiyo ni kweli. Litapona. Utaona. Sasa nenda zako, amini hayo. Nenda, amini hayo kwa moyo wako wote. Amini, dada.

²¹⁷ Sasa je! mnaamini ya kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Kama tu mtaamini,

iweni—iweni tu na imani. Mnaona? Msitilie shaka. Mnaona, “Linayatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Ni wangapi wanaojua ya kwamba Neno hufanya hivyo? [“Amina.”] Biblia, inaonyesha mmekuwa mkisoma Biblia. Sasa haidhuru uko wapi, amini sasa ule upako.

²¹⁸ Ni wangapi wameona ile picha ya Malaika wa Bwana, iliyopigwa hapa? Sasa Nuru hiyo hiyo haiko futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa hivi. Mnaona, iko kwenye kiwango kingine msichoweza kuona. Tunaishi tu katika vitano; hiki ni kingine. Sasa iweni na kicho kwa dakika moja tu.

²¹⁹ Sasa huyu hapa mama mmoja. Simjui. Sijapata kumwona. Sisi hatufahamiani, nadhani. [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Na hii ni mara yetu ya kwanza kukutana, na ni mwanamume tu na mwanamke. Na kama ningeweza kukufanyia jambo lolote, hakika ni—ningelilifanya, bali mi—mimi ni mwanadamu tu.

²²⁰ Lakini, kwa kipawa cha Mungu, ninataka kutambulisha, ninataka Yesu ajitambulishe Mwenyewe kwa Neno ambalo nimelithubiri sasa hivi, kuwaonyesha ya kwamba hii ndiyo ile saa; Neno lililogawiwa kwa ajili ya majira haya, ya kwamba tumepita kiwango cha kimadhehebu, tunajitayarisha kwenda katika Unyakuo. Ni kujaribu tu kuwapa watu imani, wapate kuamini. Mnaona?

²²¹ Ni kama tu katika yale mapi—mapiramidi, unaona, lile jiwe la kufunika ambalo kamwe halikuwa limekuja. Kwenye noti yenu ya dola, ina jambo hilo. Mnaona? Sasa hiyo huduma yenye jiwe la kufunika. Wakati ambapo ilikuwa hapa chini kabisa katika Walutheri, Wesley, na kote kote kule chini, ni ninii tu . . . Si fundisho la piramidi sasa, mnaona. Ninaonyesha tu jambo hili kwa ajili ya maelezo. Jiwe hilo la kuweka juu itabidi liwe kamilifu sana kama hayo mengine, mpaka litalandana moja kwa moja ndani yake. Huduma ya Yesu Kristo itakuwa ndani ya Kanisa Lake, kama tu Yeye hasa katika Roho, wakati atakapokuja kulichukua Kanisa, kukomboa kitu hicho chote, kisha apae juu.

²²² Je! unaamini jambo hilo? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, ninaamini.”—Mh.] Nilisema tu jambo hilo maana ninapumzika kidogo. Unaona, ni, maono ni magumu. Yule mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Naye akasema, “Naona nguvu . . .” Na huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi aliyeoko . . . Mnaona? Mnalipata? [“Ndiyo.”] A-ha. Sasa kama Bwana Yesu atanifunulia shida zako, je! utaninii . . . [“Asante, Yesu.”]

²²³ Sasa usiogope. Hilo halitakudhuru. Una hisi ya kigeni kweli, unaona. Hapo ni wakati ile Nuru ilipotulia juu yako. Sasa kama hiyo, ili kwamba watu wapate kujua, inua mkono wako juu. Kwa hiyo wewe . . . Hisi tamu kweli, ya kupendeza, unaona, unaona,

imesogea juu yako sasa hivi. Sasa usingeweza kuyaficha maisha yako hata kidogo.

224 Unaugua ugonjwa wa mapindi. Na hiyo ni kweli. [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Una mtu fulani moyoni mwako, unayemwomba. [“Ndiyo.”] Vema, bwana, huyo ni mume wako. [“Ndiyo.”] Na mume huyo ana shida na macho yake, ambayo ilisababishwa na ugonjwa wa kisukari. Na hiyo ni kweli kabisa. Unaona? Vema. Sasa, sasa amini kwa moyo wako wote, nanyi nyote wawili. . . Unaamini? Sawa, bwana. Basi, kulingana na imani yako, na iwe kwako, dada yangu. Bwana akubariki. Uwe na imani. Usitie shaka. Amini kwa moyo wako wote.

225 Sasa sisi hatufahamiani, pia, mmoja kwa mwingine. Unaamini hilo? Sasa, kusimama Mbele ya mtu kusingekufanya ujisikie hivyo. Unaona? Unajua ni kitu fulani mbali na mimi. Mimi ni kama ninii tu. . . Ni kama tu dawati lile pale, ni dawati tu. Nami ni mwanadamu tu. Lakini unaamini uko katika Uwepo Wake, si wangu; Uwepo Wake? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Asante. Mnaona? Aminini hilo kabisa, pia. Nawe huna budi kuliadini, kwa maana ninaona kivuli, unaona. Sasa huna budi kuadini.

226 Sasa unaugua matatizo ya kindani, ogani za ndani. Ulifanyiwa upasuaji. Hiyo ni kweli. Ukafanyiwa upasuaji, wala si mzuri. Ungali unakusumbua. Hiyo ni kweli kabisa. Halafu unasumbuliwa na maumivu makali ya kichwa hapa. Sasa unajua kitu fulani hakina budi kujua mambo hayo, sivyo? Unaamini sasa ya kwamba unaweza kuupokea? Unaliadini? Vema, nenda zako ukaupokee basi, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

Kila mtu sasa aombe.

227 Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia jambo ambalo unatamani? Ungeamini basi, ya kwamba kitaondoka, kifundo hicho ubavuni mwako kingeondoka? Vema, basi nenda ukaamini hilo, ndipo basi kita—kitaondoka.

228 Ninajua wewe ni mnyonge. Sitaki kukuweka zaidi ya ninavyoweza kukusaidia. Je! unaamini kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Unaamini. Mimi hunifahamu. [“Ndiyo.”] Wala hatufahamiani. Kama ningeweza kukusaidia, hakika ningekusaidia, mama. Ninge—ningetembea, nitambae, nisukume senti ishirini na tano kwa pua yangu kupitia katika barabara za mji, kukusaidia, maana wewe—wewe ni kijana, na umetiwa uvuli.

229 Ninatambua sasa, baada ya kuzungumza na wewe na kusema jambo hilo, unajua shida ni nini. Kwa hiyo unajua ya kwamba huna budi kufa mara moja usipofanyiwa jambo fulani. Una shida ya akina mama, iko katika sehemu zako za kike, na ni ya kufisha. Ni kansa. [“Ndiyo. Ndiyo.”] Nawe huna budi kufa mara moja endapo Mungu hakusaidii. [“Mwezi mmoja zaidi. . . ? . . .”—Mh.] Hiyo ni kweli. Je! unaamini ya kwamba

atakuponya? [“Ndiyo, ninaamini.”] Angalia, dada, hilo—hilo ndilo tumaini lako pekee. Amini jambo hilo sasa hivi, kwa moyo wako wote, na uuishie Ufalme wa Mungu.

²³⁰ Ninaweka mikono yangu juu ya maskini mama huyu mdogo, katika Jina la Yesu Kristo, na kumlaani ibilisi anayeyatwaa maisha yake. Naomba amwache, na jalia msichana huyu aishi, kwa ajili ya Ufalme. Amina.

²³¹ Mungu akubariki, dada. Amini sasa kwa moyo wako wote. Amini kwa moyo wako wote.

²³² Mwingine, kivuli. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuuponya na kukupa afya, akuondolee? Ulikuwa na hisi ya kigeni kabisa wakati huo uliposhughulikiwa, sivyo? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Hilo ni kweli, kwa kweli ulikuacha papo hapo. Hiyo ni kweli. Sasa amini hilo, kwa moyo wako wote, na hautakukaribia. Nenda, amini. Mungu akubariki. Vema.

²³³ Niangalie mimi, dada. Unataka kwenda kula chakula chako cha jioni na kusikia vizuri juu yake tena? Nenda zako tu. Kidonda hicho kitakuacha, nawe utakuwa mzima tena. Vema.

²³⁴ Angalia upande huu, mama. Unahofu nini? Una ugonjwa wa wasiwasi. Umekuwa ukikusumbua kwa muda mrefu. Je! unaamini Mungu anaweza kuponya wasiwasi huo na kufanya... Asilimia tisini ya wasikilizaji hawa wanatetemeka kwa kitu hicho hicho sasa hivi. Na hiyo ni kweli kabisa. Unaona? Unataka mahali pa kuweka mguu wako daima. Wewe, watu wanakwambia, “Zinduka, na uamini *hili, lile*.” Bali inakubidi kuwa na mahali pa kuanzia. Upo juu yake sasa hivi. Amini jambo hilo, utaamini? Neno la Mungu linasema wewe uko huru. Unaamini jambo hilo? [Dada anasema, “Amina.”—Mh.] Vema, nenda na ukawe huru na kitu hicho. Vema. Mungu akubariki, dada.

²³⁵ Je! unaamini Mungu anaweza kuponya kisukari na kukupa afya? [Ndugu anasema, “Naam.”—Mh.] Na unaamini? Endelea tu kusonga mbele, useme, “Asante, Bwana Yesu. Nitaenda na kuamini jambo hilo kwa moyo wangu wote.”

²³⁶ Wasiwasi, shida ya akina mama, nawe una ugonjwa wa akina mama. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza... Na ugonjwa wa tumbo, pia. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Nenda zako, ukifurahi, ukisema, “Asante, Bwana.”

²³⁷ Niangalie, bwana. Wewe ni mtu mwenye nguvu sana, bali hizo neva ni dhaifu mno. Unaamini shida hiyo itakwisha usiku wa leo? Nenda, uupokee katika Jina la Bwana Yesu. Amini kwa moyo wako wote. Naam.

²³⁸ Njoo, dada. Angalia upande huu. Naam, ninakuona ukijaribu kuamka, umelemaa karibu na kitanda. Una yabisi kavu. Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Endelea tu,

liamini, na kusema, “Yesu Kristo ananiponya,” na uliamini kwa moyo wako wote.

239 Dada yangu, je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya kisukari hicho na kukupa afya, pia? Vema. Nenda zako, ukisema, “Asante, Bwana Yesu.”

240 Njoo, mama. Yeye angetaka kukufanya uamini utakuwa wazimu. [Dada analia kwa sauti kuu, “Loo!”—Mh.] Amekuwa akikwambia hivyo, bali yeye ni mwongo. Wewe uko huru sasa. [“Ee Mungu!”] Nenda nyumbani ukafurahi, Yesu Kristo anakufanya huru. [“Loo! Ee Yesu! Yesu! Yesu! Haleluya!”]

241 Je! unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa tumbo, na kukufanya mzima? Nenda zako, ukifurahi, ukisema, “Asante, Bwana Yesu.”

242 Njoo, mama. Sasa jambo lile lile. Usiwaache wakwambie hivyo. Ni ugonjwa wa wasiwasi. Je! unaamini Mungu atakuponya, usiku wa leo? Ndilo tumaini lako la pekee la kufanya hivyo. Anza kwenda zako, ukishangilia, mwenye furaha, na kutabasamu, na uwe kama ulivyozoea kuwa. Unaona?

243 Mnaamini kwa mioyo yenu yote? Ni wangapi wanaamini sasa kwa mioyo yenu yote, “Ninaamini”? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ninaamini Yesu huokoa, na Damu Yake inaosha ikawa nyeupe kuliko theluji. Amini hayo!

244 Vipi ninyi huko nje kwa wasikilizaji, je! mnaliamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ninyi ombeni sasa, msemi, “Bwana Yesu mtu huyu yuko mbali na mimi.” Wengine wenu huku nyuma mahali fulani, vema, ombeni na mwamini.

245 Mwanamume huyu anayeketi papa hapa nyuma, ugonjwa wa kibofu nyongo. Je! unaamini Mungu ataponya kibofu nyongo na kukupa afya? Wewe, vema, imani yako, uligusa Kitu Fulani. Simjui, bali yeye aligusa Kitu Fulani. Mnaona?

246 Mama huyo anayeshangilia, karibu na wewe hapo. Je! unaamini Mungu ataponya yabisi kavu ndani yako, mama, na kukupa afya? Unaamini hayo? Vema, unaweza kuinuka... Unaweza kuupokea wako.

247 Yule anayeketi papo hapo karibu na wewe, una shida ya jicho lako. Je! unaamini Mungu ataponya ugonjwa huo wa jicho na kukufanya mzima? Vema, kama unaamini, unaweza kuponywa, pia.

248 Huyu anayeketi karibu na wewe, ana ugonjwa wa mdomo. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya uvimbe huo mdomoni mwako na kukupa afya? Unaweza kuupokea wako, pia.

249 Nawasai mwamini. Amina. Iweni na imani katika Mungu! Msitilie shaka. Aminini tu! Iweni na imani!

250 Mama anayeketi hapa, akiangalia kule nyuma kwa unyofu sana, anayeketi pale akiugua ugonjwa wa moyo. Je! unaamini

Mungu atauponya ugonjwa huo wa moyo, na kukupa afya, mama? Kama unaamini, unaweza kupata unachoomba. Naam.

²⁵¹ Sasa wewe uliyeweka lesa yako juu ya uso wako, una ugonjwa wa shingo yako na mgongo wako. Umesababishwa na ajali ya motokaa. Uligongwa kwenye motokaa, ndipo shingo na mgongo wako vikaumia. Je! unaamini utapona? Unaweza kupokea ulichoomba.

²⁵² Vipi kuhusu *humu* ndani, je! mtu fulani humu ndani anataka kuamini? Yupo mama aliyeketi pale akiniangalia, ana wasiwasi sana, ameketi moja kwa moja pale akiniangalia. Huyu anayeketi karibu naye ni mwanawe, aliye na ugonjwa wa moyo. Unaamini ya kwamba Mungu atawaponya nyote wawili. Unaamini, inua mikono yako, useme, “Ninakubali hilo.” Basi waweza kuponywa, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁵³ Tabia za Mungu humtambulisha Yeye. Je! mnaamini Yeye yupo hapa? Ni wangapi wanaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, basi. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine, basi.

²⁵⁴ Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, jalia ibilisi aliache kusanyiko hili, na jalia atupwe kwenye giza la nje.



KRISTO ALIYETAMBULISHWA KATIKA NYAKATI ZOTE SWA64-0401

(The Identified Christ Of All Ages)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 1 Aprili, 1964, katika Banda La Klabu ya 4-H huko Louisville, Mississippi, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org